SportPesa
TZS. 1,255,316,060
BET LEO UWE BILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#



UKURASA 3

**MGOMBEA** wa urais wa TLS ajitosa hoja Katiba Mpya


ama
ALHAMISI MEI 12, 2022
AFYA NA MAZINGIRA

KIKIWEKWA KANDO KINYAA... Fahamu kinyesi na mkojo wake binadamu bado hazina endelevu

AFYA YA AKILI Unajua undani wa 'Panya Road' imo katika malezi ya ubongo wa mtoto?

Mtu anapougua maradhi akili, vyanzo na shida zake hizi hapa

Na Mwandishi Wetu

MAANDIKO ya kitabu cha Kituo cha Afya cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kinatamka magonjwa ya akili yanatajwa ni matatizo ya ubongo yanayomfanya mtu kuwa na hisia, fikra na matendo tofauti na yale yanayotarajiwa na jamii, hata wakashindwa kukabiliana na magumu ya maisha.

Magonjwa ya akili yanatajwa yanaweza kusababishwa na sababu ama za kibaiolojia au kisaikolojia.

Mtu anayehisiwa kuwa na maradhi ya akili. PICHA: MAKTABA.

haraka au kupoteza kumbukumbu; kukosa uwezo wa kupambanua mambo kwa mitazamo tofauti; akijiamini ni mtu maarufu au nabii.

Mingine inajumuisha imani zisizo za kawaida kama vile kupokea taarifa redioni au kwenye mitandao ya simu; imani ya kuwasiliana na watu maarufu, kujihisi kuwa na nguvu ya ziada nje ya mwili wake; akijihisi watu wanamfuatilia kumdhuru; na mawazo yake hukosa mtiririko unaoeleweka.

MATIBABU YAKE

Matibabu ya magonjwa ya akili hutofautiana kati ya ugonjwa mmoja na mwingine. Hapo inahimizwa elimu kwa jamii kuhusiana na magonjwa ya akili, cha muhimu kusisitizwa ni kuepuka isijirudie, juu ya matibabu na mhusika awezeshwe kuendelea na maisha yake ya kila siku.

KIBAILOJIA & KISAIKOLOJIA

# Nipashe

Alhamisi Mei 12, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580943
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

UKURASA 11

# CCM, CHADEMA sasa uso kwa uso

**MBOWE** aanika kila kitu, Kina Mdee...*Endelea Ukurasa 2*



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Taifa, Freeman Mbowe (kushoto), akimkaribisha mwanasiasa maarufu kutoka Chama cha NUP cha Uganda, Robert Kyagulanyi 'Bobi Wine', baada ya kuwasili katika mkutano wa Baraza Kuu la chama hicho, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wabunge wacharuka uhaba wa ajira nchini

UKURASA 2

Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda (kushoto), akisalimiana na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna, katika viwanja vya Bunge, baada ya kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake juzi, jijini Dodoma. Prof. Mkenda ameipongeza benki hiyo kwa jitihada mbalimbali za kuboresha elimu nchini. Katikati ni Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Prof. Eliamani Sedoyeka. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



## Gari la hakimu lachomwa moto usiku

UKURASA 3

**MICHEZO** **NABI AGEUKIA SAFU YA USHAMBULIAJI YANGA** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan, akipata maelezo kutoka kwa Mwenyekiti ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda cha kutengeneza mabati na mabomba cha Roofings Ltd, Dk. Sikander Lalani, alipotembelea ili kujionea kazi za uzalishaji katika kiwanda hicho, jijini Kampala, nchini Uganda jana. **PICHA: IKULU**

# CCM, CHADEMA sasa uso kwa uso

**Na Jenifer Gilla**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, amesema atakutana na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) mwezi huu kujadili mustakabali wa siasa wa vyama vyao, kila mmoja akiwa na ujumbe wake.

Mbowe aliyasema hayo jana kwenye kikao cha Baraza Kuu la CHADEMA mkoani Dar es Salaam, akifafanua kwamba hatua hiyo ni sehemu ya makubaliano aliyofanya na Rais Samia usiku wa Jumatatu iliyopita likiwa ni ombi maalumu toka kwa Mkuu wa Nchi.

"Juzi wakati tunajiandaa kwa baraza kuu, Mheshimiwa Rais akaomba tuonane tena, nikaenda kumwona tarehe 9, tukawa na kikao cha saa mbili, akaniambia 'ninasikitika hatujakutana kama tulivyokubaliana, tafadhali tutenge muda mwingine tukutane kama tulivyokubaliana'.

"Kwa hiyo, tumekubaliana na Rais kwamba tutakutana wiki inayokuja, siyo cha Mbowe na Samia tena, bali vya 'delegation' (ujumbe) ya CHADEMA, na 'delegation' ya CCM na serikali yake, tutakwenda kuzungumza ni nini kinachofanya tunashindwa kuelewana," Mbowe alisema.

Mbowe aliongeza kuwa mkutano wa safari hii utahusisha timu ya viongozi wa CHADEMA na Serikali ya CCM ili kumaliza kile alichokiita kuponya matatizo yanayolisumbua Taifa kwa kuwa chama kimoja hakiwezi kuponya matatizo hayo'.

Alisema lengo la mkutano huo ni kuweka uhusiano wa msingi wakitambua kuwa wakiweka maelewano hayo, vyama vingine vya upinzani navyo vitafuata nyayo.

Alisema suala la yeye kuonana na Rais linaonekana ni kama miujiza kwa sababu ya kutokuaminiana kulikojengeka baina yao.

"Ziara yangu kwa Rais inaonekana ni jambo la miujiza, halipaswi kuwa hivyo, limekuwa hivyo kwa sababu nchi yetu tumejenga kutokuaminiana kwa miaka mingi, akionekana mpinzani yeyote amekwenda Ikulu, anaonekana pengine huko kuna biashara," alisema.

Mbowe alisema kuwa licha ya kupata nafasi ya kuonana na Rais saa chache baada ya kutoka jela alikokaa takribani miezi minane, alisema ilimlazimu kutumia fursa hiyo kwa maslahi ya kuileta pamoja nchi.

Mbowe pia aliitaka Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kuacha alichodai kuvigombanisha vyama hivyo kwa lengo la kuwavunja nguvu ili wakose nafasi ya kuongoza nchi.

"Ninamwambia Sisti na ninamtaka Jaji Mutungi asikie, acheni mkakati wenu wa makusudi wa kugombanisha vyama vya siasa, Ofisi ya Msajili wa Vyama haistahili kuwa chombo cha kuratibu ubatili na kututenga ili tutawaliwe sisi vyama vya upinzani," Mbowe alitamka.

Pia aliitaka ofisi hiyo iviache vyama hivyo vifanye siasa kwa uhuru bila kuingiliwa, vigombane vyenyewe na siyo kuvipangia namna ya kuendesha siasa.

"Kwa hiyo, ndugu yangu msajili tupo tayari kutoa ushirikiano kwa taasisi yako, tuko tayari kushirikiana na vyama wenzetu, tuachieni tufanye siasa kwa uhuru wetu, msitupangie namna ya kufanya siasa na nini cha kufanya katika siasa," alisema.

Mbowe pia aliwataka wanachama kuchukulia shida wanazozipitia kama fursa ya kukiimarisha chama hicho.

Wabunge viti maalum 19 wanaotokana na chama hicho, walifika kwenye Ukumbi wa Mlimani City kwa ajili ya kusikilizwa rufani yao na Baraza Kuu la chama hicho.

Wabunge hao wanaoongozwa na Halima Mdee, wanapinga kuvuliwa uanachama na CHADEMA kwa kosa la kujitokeza bungeni kuapishwa kuwa wabunge wa viti maalum kinyume cha maagizo ya chama hicho.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema, Baraza Kuu lilitarajiwa kuwa na ajenda tano, ikiwamo kusikiliza rufani ya nidhamu iliyokatwa na wabunge hao 19 wanaopinga kuvuliwa uanachama na kamati kuu ya chama hicho iliyoketi mwishoni mwa mwaka 2020.

# Ukosefu ajira vijana waibua kilio mjadala mzito bungeni

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

UKOSEFU wa ajira kwa wahitimu wa vyuo vikuu nchini jana uliibua kilio kwa baadhi ya wabunge, huku wakiitaka serikali kuandaa mtaala wa elimu utakaomjenga mwanafunzi kuwa na ujuzi wa kujiajiri.

Pia wameitaka serikali kuwekeza katika kuimarisha vyuo vya ufundi stadi sambamba na kuandaa utaratibu wa kuwapatia mitaji ya fedha wahitimu wa vyuo vikuu ili kujiajiri na kupunguza idadi ya vijana wasio na ajira mtaani.

Hoja hizo ziliibuliwa na wabunge hao wakati wakichangia hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Mbunge wa Musoma Mjini (CCM), Vedastus Manyinyi, alisema Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ndiyo mama wa kuandaa vijana katika maisha yao. Alisema vijana wengi wanamaliza shule wakiamini wataajiriwa, lakini idadi ya wanaoajiriwa ni ndogo.

"Tujitahidi kuweka nguvu katika kuboresha vyuo vya kati kuliko vyuo vya juu. Ukimchukua mtoto aliyemaliza VETA (ufundi stadi) na aliyemaliza elimu juu mwenye shahada wana utofauti mkubwa. Huyu wa VETA yuko vizuri zaidi kulikuwa wa shahada," alisema.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Esther Malleko, alisema: "Vijana wengi wanahitimu lakini hawapati ajira na hakuna mazingira ya kuwatengenezea ajira. Wanafunzi wanasomeshwa kwa mamilioni ya fedha lakini baada ya kuhitimu wanabaki nyumbani kuwa mzigo, tatizo ni kwamba elimu yetu haijawaandaa wanafunzi wetu tangu wakiwa msingi."

Alisema hivi sasa wahitimu wengi wa vyuo vikuu wanakimbilia kujiajiri kwenye kuendesha bodaboda, hali inayowapa unafuu wa kupata fedha za kujikimu kwa siku na si kujikwamua kimaisha.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Thecla Ungele, alisema: "Mtaala mpya wa elimu ulenge kuwaandaa wanafunzi wetu kwenye ufundi stadi, kilimo kuliko kuendelea kutegemea kuajiriwa."

Mussa Sima, Singida Mjini (CCM), alisema mtaala wa elimu wa sasa unazungumzia utaoaji wa elimu bora pamoja na uandaaji wa vitabu vyenye ujuzi lakini walimu wanaofundisha hawana ujuzi.

Alisema elimu inayotolewa haimwandai mwanafunzi kujiajiri, kwamba kila mwaka kuna idadi kubwa ya wanafunzi wa elimu ya juu wanaohitimu na kwenda kukaa nyumbani.

"Tuimarishe vyuo vya kati ili tupate wajuzi wengi zaidi, hii itasaidia kupunguza tatizo la ajira kwa vijana wetu, vinginevyo tutatengeneza bomu kubwa baadaye," alisema Sima.

Mbunge wa Manonga (CCM), Seif Gulamali, alisema: "Mtaala wetu ni mzigo kwa wahitimu wetu kwa sababu wanashindwa kujiajiri. Mwanafunzi wa darasa la kwanza anakuwa na masomo zaidi ya 11, tunampa mzigo tu. Mtaala uchambue masomo yawe matano au sita, tuanze kuleta uchaguzi wa masomo kuanzia elimu ya msingi.

"Mwanafunzi wa shule ya msingi tunampa vitu vingi sana, inapaswa tuwape vichache. Unakutana na mwanafunzi amebeba furushi la madaftari. Eti tunawafundisha watoto wetu binadamu alikuwa sokwe. Hivi ni kweli? Tuwape ujuzi watoto wetu wakiwa wadogo, tunawapoteza watoto wetu kusoma vitu ambavyo havina maana katika maisha yao."

Mbunge wa Mbogwe (CCM), Nicodemas Maganga, alisema mtaala wa elimu nchini bado ni changamoto. Alisema wanafunzi wengi wanahitimu lakini hawana sehemu ya kwenda.

"Unafundishwa muda mrefu kwa vitu ambavyo havina maana kisha una kwenda kushindwa katika maisha. Wanaomaliza vyuo vikuu hawana sehemu ya kwenda, nashauri wapewe mikopo na benki ili wakafanye biashara," alisema Maganga.

Mbunge wa Vunjo (CCM), Dk. Charles Kimei, alisema elimu inapaswa kuwapa ujuzi na mafunzo ya ufundi stadi wanafunzi. Alisema bado kuna tatizo katika kuwapata walimu wenye kufundisha ufundi stadi.

"Wakati tunasoma enzi hizo ukifika darasa la 12 mwalimu anakuletea fomu ya kuchagua nini ukafanye au kwenda kusomea kwenye vyuo vya maarifa au vyuo vya ufundi. Tunapaswa kujenga vyuo vya ufundi vingi ili kuondokana na tatizo la ajira," alisema Dk. Kimei.

Mbunge wa Siha (CCM), Saashisha Mafuwe, alisema mtaala unaotengenezwa sasa ujielekeze kwenye ujuzi, kwamba umruhusu mwanafunzi kusoma kitu anachotaka kuwa katika maisha yake.

Mafuwe alisema: "Mtoto anamaliza chuo kikuu hana cha kufanya, hawezi kujiajiri wala kuajiriwa. Tuangalie vipawa vya watoto ili tuviendeleze."

## HABARI KITAIFA



Mafundi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), mkoa wa kihuduma Mbagala, wakifanya matengenezo katika bomba la inchi sita katika eneo la Mbagala Rangi Tatu, ili kuimarisha upatikanaji wa huduma hiyo. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Gari la hakimu lachomwa moto

**Na Lilian Lugakingira,** MULEBA

MKUU wa Wilaya ya Muleba, Toba Nguvila, amelitaka Jeshi la Polisi wilayani humo kufanya uchunguzi na kuwakamata watu ambao hadi sasa hawajafahamika, waliochoma moto gari aina ya Harrier lenye namba za usajili T170 DFA.

Gari hilo, mali ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Mwanzo Nyamiranda, Kata ya Kyebitembe wilayani humo, lilichomwa moto usiku wa kuamkia juzi.

Akizungumza na baadhi ya wananchi wa kata hiyo katika eneo la tukio, mkuu wa wilaya huyo alisema matukio ya uhalifu katika kata hiyo yamekithiri na anasubiri kupata taarifa za kukamatwa kwa watu hao ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao.

"Wapo baadhi ya wananchi wanatoa taarifa juu ya watu waliohusika, mwenyekiti nimeishakueleza na baadhi ya namba za simu nimekupatia, ninachokitaka ni kusikia hawa watu wote waliohusika wamekamatwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria, wakipatikana tu nipewe taarifa," aliagiza.

Alisema serikali haiwezi kuacha uhalifu uendelee katika kata hiyo maana hakuna mtu ambaye yuko juu ya sheria.

"Leo limechomwa gari la hakimu, kesho litachomwa la kwako mwenyekiti wa kijiji na keshokutwa litachomwa la mtendaji, ifikie hatua watu watii sheria, vinginevyo vitendo hivi havitavumiliwa," alionya.

Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Mwanzo Nyamiranda, Emmanuel Jonathan, aliyechomewa gari lake, alidai hana ugomvi na mtu yeyote na hakuna mtu aliyejitokeza wazi kuonyesha chuki dhidi yake.

Alisema kuwa pengine tukio hilo limefanywa na watu ambao hawakuridhika na uamuzi uliotolewa katika mahakama hiyo na hivyo kuamua kuchoma gari lake moto.

"Usiku nikiwa nimelala, walikuja baadhi ya wafanyakazi wetu wakiita kwamba 'amkeni gari limechomwa moto, tokeni kwenye nyumba, nayo inaweza kuungua'. Tukaamka na kutoka nje, tukaanza kutoa baadhi ya vitu nje lakini hatukuliokoa gari maana lilikwishateketea," alisimulia Hakimu Jonathan.

Alisema kuwa baada ya kufuatilia, waligundua kuwa watu hao walipitia katika shamba la migomba kwenda kuchoma gari na baada ya kuchoma gari hilo kwa kutumia mafuta ya petroli, pia walipita katika shamba hilo kuondoka eneo la tukio.

Baadhi ya wakazi wa Kijiji Nyamiranda, akiwamo Ashura Barthazary, waliiomba serikali kuweka mikakati itakayokomesha vitendo vya uhalifu katika Kata ya Kyebitembe ili wananchi waishi kwa amani.

"Tunaishi kwa hofu, uhalifu umezidi na wanaofanya huo uhalifu hawatoki nje ya hapa, wote ni wenyeji, ni watoto wetu lakini wanafumbiwa macho.

"Hata sisi kinamama wajane tunaoishi peke yetu kwenye nyumba tunaogopa, sasa watafikia hatua ya kutuvunjia milango na kutubaka," alilalamika.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
02.05.2022

**TANGAZO**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe **04.05.2022 hadi 17.05.2022** kampuni ya **Spedag Interfreight** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Holili kuelekea Moshi,** gari hilo lenye namba za usajili: **KDB189J / ZG5310 KCW052Z / ZG3212**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| Urefu | - | Mita 28.4 |
| Upana | - | Mita 5.0 |
| Kimo | - | Mita 5.6 |

3. Njia itakayotumika: **Holili hadi Moshi kupitia Soweto,** gari litasafiri muda wa mchana tu **( Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 jioni)**

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

216843002


# Mgombea wa urais wa TLS ajitosa hoja ya Katiba Mpya

**Na Romana Mallya**

WAKILI Harold Sungusia, ametaja sababu tatu zilizomfanya kugombea nafasi urais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) kubwa likiwa ni ajenda ya kitaifa iliyopo hivi sasa ya Katiba Mpya.

Akizungumza katika mahojiano yaliyofanyika hivi karibuni, Wakili Sungusia alisema mawakili huwa na mambo mengi yanayowahusu kuhusiana na haki zao za msingi.

"Mawakili wa miaka ya nyuma wamekuwa wakichanganywa na wateja wao wakati mwingine, vyote hivyo vinaonyesha kutokuwapo na uthabiti kwenye utawala wa sheria, huwezi ukawa na utawala wa sheria, katiba hailindi na kulea utawala wa sheria," alisema. Alisema kwa sasa kuna ajenda ya katiba na miongoni mwa mambo ya msingi na fursa kwa mawakili wote ni kutoa uongozi kwenye suala linalohusiana na taifa.

"Hasa kazi kubwa ya mawakili kwa mujibu wa kifungu cha 4 cha sheria iliyoanzisha Chama cha Mawakili ni pamoja na kusaidia umma na kuwalinda wananchi wa kawaida dhidi ya ukandamizaji wowote na kuishauri na kuisaidia serikali katika masuala yanayohusu sheria na mahakama katika masuala yote ya sheria," alisema.

Pia alisema pamoja na yote ni kusaidia, kuwalinda na kuwawezesha wanachama wake ambapo suala lililoibuka la kitaifa kwa sasa linahitaji mchango mkubwa wa mawakili.

Wakili Sungusia alisema si mchango wa mtu mmoja kwa kuwa ni ajenda ya kitaifa basi kuwe na vikao vya mara kwa mara vya mawakili wakielezwa, wakijadili na kuamua nini cha kufanya na kutoa uongozi unaohitajika. "Si suala la timu au kamati au kikosi kuamua, ni suala la wanachama kuamua, lakini TLS kinatakiwa kitoke na muafaka, hili ni la kwanza," alisema.

Sungusia alitaja jambo la pili lililomfanya agombee ni suala zima la maslahi ya wanachama ambapo amefanya kazi kwenye asasi zisizo za kiserikali kwa zaidi ya miaka 15 na kusaidia kutunisha mifuko ya taasisi alizofanya nazo kazi.

Alisema anataka wafanye miradi mikubwa ambayo itaingiza fedha kwa taasisi na mawakili ili ilete tija kwa wananchi.

"Tunataka tutunishe mifuko yetu mawakili wafanye kazi, tuache kulialia njaa. Jambo la tatu, suala la TLS mwisho wa siku kuwe na uendelevu wake.

Tuna wanachama tunakaribia 10,000 na wengi ni vijana na taasisi imekuwa kubwa sasa nini kifanye kupunguza gharama za kuendesha chama kwa sababu ni kikubwa na nini kifanyike kutumia hii fursa ya wingi huu wa wanachama ili chama kidumu," alisema.


TATEPA
TATEPA LIMITED

**NOTICE OF ANNUAL GENERAL MEETING**

Notice is hereby given that the 28th Annual General Meeting of the Company in respect of the year ended 30th September 2021 will be held at hotel Slipway Conference Centre, Slipway road, Msasani peninsula Dar es salaam on **Thursday the 26th May 2022 at 11:30 AM EAT**

**AS ORDINARY BUSINESS**

1. Confirmation of the Minutes of the 27th Annual general meeting held on the 29th April 2021 at the courtyard hotel, ocean road, Dar es salaam.

2. To receive, consider and adopt the report of the board of directors, the audited financial statements for the year ended 30th September 2021, and the report of the auditors' thereon.

3. To approve no payment of dividend for the year 2020-21 as recommended by the board of directors of the company.

4. To appoint and re- appoint the following directors for a period of two (2) years:
   a) Mr. George Carmichael Theobald - chairman
   b) Mr. Johannes Gunnell
   c) Mr. Robin Harrison
   d) Mr. Hendrik Andries De Klerk
   e) Mr. Edward Stiles
   f) Mr. Ran Kadoch
   g) Mr. David Bulengo
   h) Mr. Alexander Puxley

5. To appoint Baker Tilly DGP & Co, IT plaza, 10th floor, phone No. +255 653 222 299 Ohio street, Dar Es Salaam, as the company auditors as recommended by the board of Directors for the financial year 2020-21.

6. Any other business

A member entitled to attend and vote at the Annual General Meeting is entitled to appoint any person (whether a member of a Company or not)

216850902

# Wasafirishaji wampa tano Samia kukabili kupanda gharama maisha

Na Mwandishi Wetu

CHAMA cha Wasafirishaji Tanzania (TAT) kimempongeza Rais Samia Suluhu Hassan na serikali yake kwa hatua inazochukua kukabiliana na kupanda kwa gharama za maisha kunakotokana na wimbi la kupanda kwa bei ya mafuta duniani.

TAT yenye wanachama wasafirishaji wa mizigo na mafuta zaidi ya 200, imekuwa kikifuatilia kwa karibu mwenendo wa mabadiliko ya bei za mafuta nchini na changamoto zake kwa kuwa athari zake zinaigusa moja kwa moja kutokana na magari ya wanachama wake husafirisha kila siku bidhaa ndani na nje ya mipaka ya Tanzania.

Msemaji wa TAT, Omar Kiponza, alisema jana katika taarifa ya chama hicho kwamba changamoto zote zinazowakabili Watanzania na sekta ya usafirishaji, ufumbuzi wake utapatikana kwa kutumia busara na hekima inayoonyeshwa na Rais Samia na serikali nzima.

"Pamoja na kupanda kwa bei ya mafuta, katika siku za karibuni yamekuwapo matukio ya migomo ya madereva na sintofahamu kadhaa ndani ya sekta ya usafirishaji, TAT inaamini kwamba yote hayo yatatatuliwa kwa kuyakabili kama Watanzania tunaopenda na kuitakia mema nchi yetu," alisema Kiponza.

Rais wa TAT, Mohamed Abdullah, alisema ni wako wasafirishaji wachache wenye changamoto na pia kuna baadhi ya madereva ambao wana matatizo, lakini yote haya yanaweza kumalizwa kwa kukumbuka kwamba wote ni Watanzania na rabsha katika sekta ya usafirishaji zinaipaka tope nchi, serikali na Watanzania wote.

"Serikali inaendelea kushughulikia suala la bei za mafuta na haya mambo ya migomo ya madereva na kero za baadhi ya wasafirishaji. Tuipe muda na tuwe na subira. Tunampongeza Rais Samia na serikali kwa hatua inazochukua.

"Unaweza kusema haya yanayotokea sasa ukiacha mafuta kupanda, ni mambo yasiyo ya afya kwa sekta ya usafirishaji na kwa nchi yetu. Kuna baadhi ya madereva wanatumiwa. Nia ni kudhoofisha Bandari ya Dar es Salaam, sekta ya usafirishaji na uchumi wa nchi yetu," alisema.

Abdullah aliongeza kuwa: "Madereva ni ndugu zetu, kama kuna stahili zao wapewe. Wasafirishaji wanaopindisha haki waache mara moja na sote kwa pamoja tujihadhari na chokochoko za kutoka nje ya nchi zenye malengo ya kutufanya tugombane wenyewe kwa wenyewe kwa faida ya watu na biashara za nje."

Juzi, serikali kupitia Waziri wa Nishati, January Makamba, ilitangaza hatua kadhaa za kukabili kupanda kwa bei za mafuta zikiwamo ruzuku ya Sh. bilioni 100 na ruksa kwa wafanyabiashara wenye mitaji kuingiza mafuta.

Hatua zingine ambazo serikali imetangaza kuzichukua katika kukabiliana na tatizo hilo ni kuanzisha mfuko wa kuhimili ukali wa bei za mafuta; kuanzisha hifadhi ya mafuta ya kimkakati; kuanzisha upokeaji wa mafuta katika ghala moja; na kuimarisha taasisi zinazohusika na suala la mafuta.




Naibu Waziri wa Madini, Dk. Steven Kiruswa (katikati) akishuhudia Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Madini Tanzania (STAMICO), Dk. Venance Mwasse (kushoto), akibadilishana hati na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya ABSA Commodities ya Uswisi, Gerges Schmickrath, jijini Dodoma juzi, baada ya kutiliana saini mkataba wa miaka mitano ya uchimbaji makaa ya mawe mkoani Songwe. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# ACT yabainisha shida nane elimu

Na Halfani Chusi

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimeainisha vikwazo vinane vinavyoikabili sekta ya elimu nchini, hivyo kusababisha kuwapo mijadala mingi kuhusu sekta hiyo.

Msemaji wa Sekta ya Elimu wa ACT-Wazalendo, Riziki Shahari Mngwali jana mkoani Dar es Salaam, alibainisha vikwazo hivyo jana alipozungumza na waandishi wa habari, akisisitiza vinadidimiza ukuaji wa elimu nchini.

Alisema kutokana na umuhimu wa elimu, bajeti ya sekta ya elimu imekuwa ikifuatiliwa na wananchi na wadau mbalimbali, wakiomba vipengele kadhaa kufanyiwa marekebisho.

"Kwa hiyo niseme tu kuna maeneo manane ambayo ACT-Wazalendo imeona kama serikali isipoyafumbia macho, basi tutakuwa tumeboresha elimu yetu kwa kiasi kikubwa.

"Mambo yenyewe; Usimamizi duni wa utoaji wa elimu ya awali, msingi na shule za upili nchini; wanafunzi kukatisha masomo kabla ya kumaliza elimu ya msingi; udhibiti na ubora katika elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi hayapewi kipaumbele nchini.

"Hakuna elimu bila walimu, serikali imalize tatizo la uhaba wa walimu; Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu inaendeleza ubaguzi katika mfumo wetu wa elimu; mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya miradi ya maendeleo ya elimu; haki ya elimu kwa mtoto wa kike; pamoja na elimu ya mafunzo ya vitendo kwa elimu ya juu."

Riziki pia aliikosoa serikali kwa kusuasua kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Elimumsingi Bila Malipo, maarufu elimu bure, pia alichokiita ulegevu katika utoaji huduma za elimu na ujenzi wa miundombinu ya elimu.

"Mwaka 2016 serikali ilianza kutekeleza mpango wa elimumsingi bila malipo, huu ni mkakati mzuri wa serikali kuhakikisha watoto wote wa Kitanzania wanapata elimu ya msingi bila kikwazo cha ada.

"Hata hivyo, takwimu zinaonyesha kuna upungufu mkubwa sana wa walimu kuanzia ngazi ya awali, shule za msingi na upili, pia kuna upungufu wa vyumba vya madarasa na vitabu, hivyo kwa muda mrefu serikali imeshindwa kufanya ukaguzi wa ufanisi kwenye shule za msingi na upili ili kukagua na kudhibiti ubora wa elimu inayotolewa," alifafanua.

Aliishauri serikali kuhakikisha kila mtoto wa kike aliyepata mimba akiwa shuleni, anamaliza elimu yake kama ilivyokusudiwa kwa kusimamia ahadi ya kuruhusu kumrejesha mtoto wa kike shuleni.

## Gari la hakimu lachomwa moto

Na Lilian Lugakingira, MULEBA

MKUU wa Wilaya ya Muleba, Toba Nguvila, ameliitaka Jeshi la Polisi wilayani humo kufanya uchunguzi na kuwakamata watu ambao hadi sasa hawajafahamika, waliochoma moto gari aina ya Harrier lenye namba za usajili T170 DFA.

Gari hilo, mali ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Mwanzo Nyamiranda, Kata ya Kyebitembe wilayani humo, lililochomwa moto usiku wa kuamkia juzi.

Akizungumza na baadhi ya wananchi wa kata hiyo katika eneo la tukio, mkuu wa wilaya huyo alisema matukio ya uhalifu katika kata hiyo yamekithiri na anasubiri kupata taarifa za kukamatwa kwa watu hao ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao.

"Wapo baadhi ya wananchi wanatoa taarifa juu ya watu waliohusika, mwenyekiti nimeishakueleza na baadhi ya namba za simu nimekupatia, ninachokitaka ni kusikia hawa watu wote waliohusika wamekamatwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria, wakipatikana tu nipewe taarifa," aliagiza.

Alisema serikali haiwezi kuacha uhalifu uendelee katika kata hiyo maana hakuna mtu ambaye yuko juu ya sheria.

"Leo limechomwa gari la hakimu, kesho litachomwa la kwako mwenyekiti wa kijiji na keshokutwa litachomwa la mtendaji, ifikie hatua watu watii sheria, vinginevyo vitendo hivi havitavumiliwa," alionya.

Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Mwanzo Nyamiranda, Emmanuel Jonathan, aliyechomewa gari lake, alidai hana ugomvi na mtu yeyote na hakuna mtu aliyejitokeza wazi kuonyesha chuki dhidi yake.

Alisema kuwa pengine tukio hilo limefanywa na watu ambao hawakuridhika na uamuzi uliotolewa katika mahakama hiyo na hivyo kuamua kuchoma gari lake moto.

"Usiku nikiwa nimelala, walikuja baadhi ya wafanyakazi wetu wakiita kwamba 'amkeni gari limechomwa moto, tokeni kwenye nyumba, nayo inaweza kuungua'. Tukaamka na kutoka nje, tukaanza kutoa baadhi ya vitu nje lakini hatukuliokoa gari maana lilikwishateketea," alisimulia Hakimu Jonathan.

Alisema kuwa baada ya kufuatilia, waligundua kuwa watu hao walipitia katika shamba la migomba kwenda kuchoma gari na baada ya kuchoma gari hilo kwa kutumia mafuta ya petroli, pia walipita katika shamba hilo kuondoka eneo la tukio.

Baadhi ya wakazi wa Kijiji Nyamiranda, akiwamo Ashura Barthazary, waliiomba serikali kuweka mikakati itakayokomesha vitendo vya uhalifu katika Kata ya Kyebitembe ili wananchi waishi kwa amani.

"Tunaishi kwa hofu, uhalifu umezidi na wanaofanya huo uhalifu hawatoki nje ya hapa, wote ni wenyeji, ni watoto wetu lakini wanafumbiwa macho.

"Hata sisi kinamama wajane tunaoishi peke yetu kwenye nyumba tunaogopa, sasa watafikia hatua ya kutuvunjia milango na kutubaka," alilalamika.

HABARI KITAIFA

# Mahakama Kuu yayatupa maombi wafanyakazi TPA

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Kazi imetupilia mbali maombi ya waliokuwa wafanyakazi 16 wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) ya kutaka kukatishwa kwa mikataba yao kusikilizwa na Baraza la Usuluhishi Temeke (CMA) kwa sababu hawana vigezo vya kupeleka malalamiko yao huko.

Uamuzi huo ulitolewa na Jaji Biswalo Mganga wa mahakama hiyo baada ya kupitia hoja za pande zote mbili, akisema hakuna ubishi kwamba TPA wanahusika na vitu muhimu vinavyogusa masuala ya usalama wa nchi.

"Hivyo, wafanyakazi hawawezi kuchukuliwa kuwa siyo watumishi wa umma. Moja ya majukumu ya TPA ni kuiweka bandari salama chini ya Kifungu namba 5(d), hii ni muhimu kwa ustawi wa Taifa," alisema.

Jaji Mganga alisema kulingana na hoja zilizowasilishwa na mawakili wa serikali, Rehema Mtulya (TPA) na Mwantumu Self, ni kwamba walalamikaji walisitishiwa ajira wakati serikali ikifanya uhakiki wa vyeti vya taaluma. Alisema hashawishiki na hoja za walalamikaji kwamba siyo watumishi wa umma, hivyo walitakiwa na wanatakiwa kupeleka malalamiko yao katika Tume ya Utumishi wa Umma na siyo kuyapeleka CMA.

"Kwa maneno mengine walalamikaji hawana vigezo vya kupeleka malalamiko CMA kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, kwa hiyo CMA hawana mamlaka ya kusikiliza malalamiko na ninaendelea kusimamia uamuzi wa CMA," alisema.

Akiwasilisha hoja, Wakili wa walalamikaji, Stella Simkoko alidai kuwa wateja wake walisitishiwa ajira zao mwaka 2018 na kwamba CMA ilikuwa na mamlaka ya kuwasikiliza chini ya kifungu 3(a)(ii) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298 ya mwaka 2019.

Aliendele kudai kwamba kwa mujibu wa sheria, mlalamikiwa ni shirika linalomilikiwa na serikali lakini wafanyakazi wake siyo watumishi wa umma.

Aliendelea kujenga hoja kuwa shirika la umma ni tofauti na taasisi ya umma kwa mujibu wa sheria ya mashirika ya umma ambayo inaziondoa taasisi za umma kwenye mashirika hayo, hivyo inawapa uhalali walalamikaji kupeleka malalamiko yao CMA.

Alidai mwaka 2019 Sheria ya Bandari ilifanyiwa marekebisho ambapo kifungu cha 38A kiliongezwa ambacho kinasema kwamba mamlaka kwa ruhusa ya wizara inaweza kufanya uamuzi unaohusiana na huduma za wafanyakazi kwa kusimamia Sheria ya Utumishi wa Umma.

Simkoko alidai kuwa kabla ya marekebisho ya sheria walalamika hawakuwa chini ya sheria ya utumishi wa umma, hivyo CMA na mahakama wote wana mamalaka ya kusikiliza.

Akijibu hoja hizo, Wakili Mtulya alidai CMA na mahakama wote hawana mamlaka na kuongeza kuwa Sheria ya Mamlaka ya Bandari Na. 17 ya 2004 kifungu cha 4(1)(a) inaeleza Mamlaka ya Bandari ni shirika la umma. Aliendelea kudai kuwa walalamikaji walisitishiwa ajira mwaka 2018 na hati iliyoidhinishwa na serikali, hivyo walitakiwa kupeleka malalamiko kwa mujibu wa sheria ya utumishi kabla ya kwenda CMA, hivyo CMA hawana mamlaka ya kusikiliza malalamiko hayo. Septemba 15 , 2018, TPA (mdaiwa) ilikatisha mikataba ya wafanyakazi 16 ambao ni Charles Daudi na wenzake 15.

Kutokana na kusitishwa kwa mikataba yao, walalamikaji walikwenda kufungua shauri katika Baraza la Usuluhishi Temeke.

TPA waliwasilisha pingamizi la awali kwamba CMA haina mamlaka ya kusikiliza shauri hilo kwa kuwa wafanyakazi hao walikuwa watumishi wa umma.

Mei 21, 2019, baraza hilo lilisikiliza pingamizi hilo ambapo CMA ilikubaliana na pingamizi hilo, walalamikaji waliomba waongezwe muda ili wafungue maombi ya kuomba mapitio ya uamuzi huo katika Mahakama Kuu ya Kazi. Maombi ya wafanyakazi hao yalikubaliwa na walipewa siku 14. Februari 24, 2022 Mahakama Kuu ilikubali maombi yao na kuwapa siku 14 za kuwasilisha maombi yao ya mapitio kwamba hawana vigezo vya kuwasilisha shauri lao CMA.

# Chanjo polio kuwafikia watoto milioni 10 nchini

**Na Mary Geofrey**

CHANJO ya ugonjwa wa Polio kwa watoto walio na umri chini ya miaka mitano inatarajiwa kuanza kutolewa nchini Mei 18 hadi 21 mwaka huu.

Utoaji huo wa chanjo utakuwa kwenye mfumo wa kampeni itakayofanyika nyumba kwa nyumba, mtaa kwa mtaa, masokoni na maeneo ya mikusanyiko kwa lengo la kufikia watoto 10,567,805 wenye umri huo.

Ofisa Programu Mpango wa Taifa wa Chanjo Wizara ya Afya, Lotalis Gadau, akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, alisema kampeni hiyo itasaidia kuzuia kuenea kwa ugonjwa huo ambao unashambulia viungo vya mwili na kusababisha ulemavu wa kudumu au kifo.

Alisema kampeni itafanyika kwa awamu tatu kuanzia Mei, Juni na Julai na kuhusisha wasimamizi wa kitaifa katika mikoa yote.

Gadau alisema kampeni hiyo itahusisha makundi matatu ya wahamasishaji, watoa chanjo na wakaguzi wa kuhakiki kama kuna mtoto ambaye hajapata chanjo hiyo.

Alisema kila mtoto atakayepatiwa chanjo hiyo, atawekewa alama ya wino kwenye kidole kidogo cha mwisho ambayo inafutika baada ya wiki ili kuonyesha amepata huduma. Alifafanua kuwa ugonjwa wa polio kwa miaka mingi umekuwa tishio kwa nchi nyingi duniani ikiwamo Tanzania na kwa mara ya mwisho mgonjwa wa aina hiyo kupatikana nchini ni Julai mwaka 1996.

"Hivi karibuni Malawi ilitoa taarifa ya mgonjwa wa polio, Februari 17, mwaka huu na kutokana na mwingiliano wa wananchi baina ya Tanzania na nchi hiyo, tathmini iliyofanyika na Wizara ya Afya na Shirika la Afya Duniani (WHO), nchi yetu ilionekana miongoni mwa nchi zilizo katika hatari ya kupata maambukizi hayo endapo hatua madhubiti hazitachukuliwa," alisema.

Ugonjwa huu hauna tiba, unaweza kuzuiliwa kwa kupata chanjo ya matone au sindano na ili kujikinga ni vyema kupata chanjo ambayo kwa sasa itatolewa kwa watoto wote wenye umri chini ya miaka mitano," alisema Gadau. Alitaja viashiria vya ugonjwa huo ni pamoja na ulemavu wa ghafla, kulegea kwa viungo, kukosa nguvu, kushindwa kunyanyua mguu au mkono, mtoto kushindwa kukaa, kushindwa kutembea na kuvuta miguu.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**OMBI LA KUONESHA NIA KWA AJILI YA UTOAJI WA HUDUMA ZA UOKOZI NA MATIBABU, TANZANIA**
**KUMBUKUMBU NO: 10007711**

Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), kampuni ya mafuta na gesi, inaalika mashirika yenye uzoefu na yanayoheshimika kuonesha nia ya kutoa huduma za uokozi na matibabu kwa EACOP.

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 296 ziko Uganda na 1,147 ziko Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:**

**Mawanda ya kazi/utaratibu wa program ya kutoa huduma ya uokozi na matibabu**

1. Kutathimini miundombinu ya afya kwenye mkuza wa bomba la mafuta na na njia za usafirishaji mtoa huduma atatakiwa kufanya ukaguzi halali na wa uhakika kwa kila sehemu (site) ambao utatathimini juu ya uwezo wa miundo mbinu.
2. Kufanya tathmini ya ndege iliyopo ya uokoaji itakayotumika wakati wa uokozi. Kupitia na kutathmini watoa huduma za kusafirisha na muda wa uokozi wa ndani ya nchi na nje ya nchi, ikihusisha na tathmini ya mpango na manajiment ya barabara za ndani, na uwezo wa uokozi kwa njia ya anga kwenye bomba la mafuta.
3. Uundaji wa suluhisho mahususi la Usaidizi wa Kimatibabu ambalo litamwezesha Mtoa Huduma kuunga mkono uratibu wa Huduma za Uokoaji wa Matibabu kulingana na utaratibu wa kawaida wa kufanya kazi, ikijumuisha uundaji wa mpango wa Mradi wa uokoaji wa matibabu (MEDEVAC).
4. Mawanda ya hiari-Utekelezaji na usimamizi wa vituo vya matibabu kwenye maeneo yote ya kazi za mradi:

- Utoaji wa usimamizi wa Mnyororo wa Ugavi wa Matibabu
- Usimamizi wa Vifaa vya Matibabu vya Mkandarasi kwenye Maeneo husika
- Wafanyakazi na kuendesha klininiki za wakandarasi
- Utoaji wa huduma za usimamizi wa ubora wa matibabu
- Utoaji wa huduma za afya kazini
- Huduma za Kinga na afya ya umma
- Utoaji na ushauri, ukaguzi na uwezo wa utaalam
- Huduma za afya ya jamii
- Utoaji wa matibabu kwa njia ya teknolojia ya mawasiliano.

**VIGEZO MUHIMU:**

Makampuni inayotaka kuonyesha nia yanatakiwa kuwa na vielelezo vifuatavyo:

- Leseni ya Biashara.
- Uthibitisho wa kusajiliwa na mamlaka ya mapato Tanzania (TRA) na cheti kinachoonyesha uthibitisho ulipaji wa kodi kwa mwaka wa hivi karibuni.
- Uthibitisho wa kusajiliwa katika kanzi data ya EWURA (LSSP) au uthibitisho wa maombi ya kusajiliwa wakati wa kuwasilisha nia yake ni muhimu sana.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani
- Uzoefu wa wa utoaji wa huduma ya uokozi na matibabu kwenye miradi inayofanana na mradi wa EACOP katika ukubwa, mawanda na kijiografia.
- Umahiri na uwezo katika kutoa Huduma za Uokoaji wa Matibabu kama ilivyoainishwa hapo juu kwa kiwango kikubwa, kwa kuzingatia viwango vya kitaifa na kimataifa, na kwa uzoefu wa angalau miaka 10/utendaji wa huduma kama hizo.
- Wafanyakazi waliohitimu na wenye uzoefu katika kutoka huduma za Uokoaji/uokozi na matibabu kwa miradi ya mafuta na gesi ambayo inatii mahitaji ya IFC.
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha hesabu za fedha za muda wa miaka mitatu iliyopita.
- Uthibitisho wa sera ya ndani ya Ubora, Afya, Usalama mahala pa kazi na Mazingira (QHSE), taratibu na mchakato kulingana na viwango vya ndani ya viwanda vya kazi husika.
- Uthibitisho wa kupambana na rushwa na sera za ufuatiliaji
- Uthibitisho wa leseni unaofaa kutoka kwa mamalka husika ndani ya nchi kwa ajili ya huduma

Makampuni yenye nia ya kuleta maombi na ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizoorodheshwa hapo juu zinapaswa kueleza nia yao kwa kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **procurement.tz@eacop.com** saa au kabla ya saa **10 jioni** za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **27th May 2022.** Ukubwa wa barua pepe usizidi **20Mb.** Taarifa zote ziwasilishwe kwa lugha ya Kingereza

**Muhimu:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazoonyesha nia ili kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Makampuni ya awali yenye vigezo ndiyo yatakayopokea mrejesho. Taasisi zitakazokidhi vigezo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni.

Nipashe

MWANGA WA JAMII

# Mpango utoaji mikopo elimu ya juu uboreshwe

**JUZI** Bunge liliagiza serikali kuangalia upya vigezo vya utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu, ili kupunguza malalamiko ya kutokuwa na vigezo vya ulinganifu yanayojitokeza mara kwa mara miongoni mwa waombaji na wazazi.

Pia liliagiza serikali kuhakikisha Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) inaanza kujiendesha kibenki ili kuwezesha na kurahisisha utoaji na ukusanyaji wa mikopo kwa wanafunzi wanaohitaji mikopo.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Aloyce Kamamba, alitoa ushauri huo wakati akiwasilisha bungeni maoni, ushauri na mapendekezo kwa makadirio ya mapato na matumizi Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2022/23.

Alisema serikali iangalie uwezekano wa kuwapatia mikopo wanafunzi wa elimu ya kati pamoja na kuangalia upya vigezo vya utoaji wa mikopo ya elimu ya juu. Alisema hatua hiyo itapunguza malalamiko ya kutokuwa na vigezo vya ulinganifu yanayojitokeza mara kwa mara.

Sambamba na hilo, alishauri serikali kuendelea kutafuta vyanzo vya fedha ili kuwapatia mikopo wanafunzi wote wanaohitaji mikopo na kwamba ni muhimu bodi ikajiendesha ili kurahisisha utoaji wa mikopo na ukusanyaji wa mikopo kwa wanafunzi wanaohitaji.

Malalamiko ya mikopo yamekuwapo kwa muda mrefu kwamba wanaostahili kupata hawapati, huku wakiwamo ambao wazazi wao wanaweza kuwasomesha lakini wanapewa mikopo.

Wako wanafunzi ambao ni yatima kwa maana ya kwamba hawana baba wala mama, au wametoka kwenye familia maskini lakini wanapoomba mkopo ili waendelee na masomo, wamejikuta wanapata asilimia ndogo huku wenye uwezo wakipata asilimia kubwa.

Wanafunzi wengi wamejikuta wanataabika kwa kuishi maisha magumu, wengine wakishindwa kufanya mtihani kwa sababu hawajalipa ada kiasi cha wadau kuwachangia ili kuendelea na masomo.

Aidha, wazazi wengi husomesha watoto wao kwenye elimu ya msingi na sekondari kwa jasho, wakiamini wakifika chuo kikuu watapata mkopo na itapunguza maumivu, lakini wapo walioshindwa kuendelea na elimu ya juu kwasababu ya kukosa mkopo.

Utoaji wa mikopo umelalamikiwa kwa muda mrefu na watu wengi kwamba hautoi haki sawa kwa wote wanaostahili kupata mikopo, na ndiyo maana wengi wameachwa wakaishi maisha magumu au wengine wakakosa nafasi za kusoma.

Tunaishauri serikali kuliangalia jambo hilo kwa kina, kufanya utafiti wa kina utoaji wa mikopo ili wenye sifa pekee wapate kulingana na matakwa.

Wako waliosomeshwa vizuri na wazazi wao lakini baadaye walifariki dunia au kufilisika wakashindwa kuendelea kusomesha watoto wao, ndiyo maana kumekuwa na kilio cha mikopo kutolewa kwa wote bila ubaguzi.

Wengi wamesema ni muhimu kila mwanafunzi anayeomba mkopo apewe, huku wakienda mbali hadi kwa wenye elimu ya kati ambayo ina wanafunzi wengi.

Pia ni muhimu kuweka mifumo mizuri zaidi ya kurejesha fedha hizo, ikiwamo serikali kuendelea kutengeneza ajira zaidi kwa wanaomaliza vyuo, pia kuwa na mitaala itakayozalisha watu wanaoweza kutengeneza ajira badala ya kutegemea kuajiriwa ambako ni changamoto kubwa kwa sasa.

Inawezekana bodi inaelemewa kwa kuwa fedha zinatoka lakini uwezo wa kurejesha ni mdogo, kwa kuwa wengi wanamaliza vyuo hawana ajira na uwezo wa kurejesha deni hilo ambalo linaongezeka kadri muda unavyosonga.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Halfani Chusi

# Kupanda bei ya mafuta mtaani kumebadili ghafla mkao wetu

**BEI** ya mafuta kwa sasa ipo juu na sasa imeongeza gharama kwa wananchi kwa kuongezeka kasi ya ugumu wa maisha, kwa kiwango kikubwa kutokana na bei za bidhaa au kwa lugha rahisi mfumuko wa bei.

Watanzania wengi wamejiajiri katika kuendesha vyombo vya moto kama vile Bajaji na Bodaboda, ili kujipatia kipato cha kuendesha maisha yao ya kila siku.

Kwa hiyo, kupanda bei ya mafuta kumewaathiri wengi, lakini kikubwa zaidi ni hilo la kuongezeka kwa bei kwa baadhi ya vyombo vya usafiri kama vile daladala, Bajaji na Bodaboda.

Kwa mtazamo wangu, suala la kupanda bei za nauli kwa vyombo vya usafiri kupitia ongezeko la bei ya mafuta limeongeza kwa kasi, ugumu wa maisha huko mitaani tuliko na kwingineko.

Kupitia gharama za usafiri kuwa juu, bei ya vitu navyo imekuwa juu hasa sokoni kunakopatikana vyakula, ukweli ni kwamba hata unapododosa nini shida, mrejesho kutoka kwa wauzaji ni kwamba wanasafirisha bidhaa hizo kwa gharama kubwa sana, ikichagizwa na kupanda gharama za mafuta ya vyombo vya usafiri.

Maumivu ni makubwa mno kwa watu wenye vipato vidogo na Waswahili wanasema, kipato kwa sasa hakikidhi mahitaji, kwa maana ya kuwa kinachopatikana hakimudu gharama za matumizi.

Lakini, linaloleta faraja ni pale timu ya kiserikali kwa kuanzia na mkuu wa nchi, Rais Samia Suluhu Hassan kuchukua hatua, ipo mbioni kutupunguzia makali hayo.

Katika hili nasema, ni jambo la heri na muhimu, kwani litawasaidia Watanzania wote na hasa wenye vipato vidogo katika jitihada za kumudu mahitaji na kurejesha tumaini jipya la mtaani ambako kuna kundi kubwa la umma.

> **Mbali na ongezeko la nauli katika vyombo vya usafiri kutokana na kupanda kwa bei, pia katika pembejeo za kilimo, kwa sasa hali nayo ni mbaya zaidi kulinganisha na miaka ya nyuma, huku baadhi ya wafanyabiashara wa pembejeo hizo wakisingizia kupanda kwa gharama za usafirishaji wa bidhaa hizo.**

Rai yangu kwa serikali ni kuharakia kushuka kwa bei ya mafuta, kwa kuwa hali ni mbaya mtaani kwa kufanya hivyo kutapunguza gharama za maisha na kuongeza mzunguko wa pesa mtaani.

Angalau niwarejeshee tena lugha ya ahsante, kwa kile kinachotajwa kutekelezwa kuanzia wiki tatu zijazo.

Mbali na ongezeko la nauli katika vyombo vya usafiri kutokana na kupanda kwa bei, pia katika pembejeo za kilimo, kwa sasa hali nayo ni mbaya zaidi kulinganisha na miaka ya nyuma, huku baadhi ya wafanyabiashara wa pembejeo hizo wakisingizia kupanda kwa gharama za usafirishaji wa bidhaa hizo.

Ukiangalia hapo kuna kundi kubwa la wakulima linashindwa kukabiliana na gharama za pembejeo za kilimo zikiwemo mbegu, mbolea na dawa kwa ajili yake.

Ni hali inayowafanya wakulima washindwe kulima na wengine hawawezi kuzalisha mazao bora yatakayoleta changamoto ya ushindani kutunadi katika soko la kimataifa na kwingineko.

Kwa ujumla, tukiangalia suala hilo la kupanda kwa gharama za mafuta kwa mapana yake, limewaathiri wengi na mambo yamekuwa magumu zaidi kila sekta, kutokana na maeneo mengi ya uzalishaji nchini kwetu kutegemea usafirishaji kwa asilimia kubwa

# Muhimbili yapokea vifaa vya mamilioni

Na Romana Mallya

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH) imepokea msaada wa vifaa vyenye thamani ya Sh. milioni 139.7 kutoka kwenye timu ya madaktari waliotokea Jimbo la Shangdong, China ambao kwa sasa wanatoa huduma nchini.

Timu hiyo ya madaktari 10 ambao ni wataalamu katika maeneo tofauti ya afya, ipo nchini kwa muda wa miaka miwili na wanafanya kazi ya kutoa huduma katika hospitali nne ikiwamo Muhimbili.

Akizungumza jana baada ya kupokea msaada huo, Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Prof. Lawrence Museru, alisema kwa miaka 40 Muhimbili imekuwa ikipokea wataalamu kutoka China katika maeneo ambayo hospitali haijajitosheleza.

Alisema kwa sasa wamepokea madaktari wanne kutoka katika timu hiyo wanaotoa huduma katika vitengo cha usingizi, wagonjwa mahututi na upasuaji wa watoto.

"Madaktari wengine wawili wapo Taasisi ya Jakaya Kikwete (JKCI), wawili Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI) na wawili Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya.

"Katika utoaji huduma wameona kuna maeneo vifaa havijajitosheleza, hivyo wamevileta ili kuboresha huduma zetu za matibabu," alisema.

Alisema thamani ya vifaa ambavyo vipo 18 ni Sh. milioni 139.7 na kwamba vitatumika hospitalini hapo kwa wagonjwa mahututi na maeneo mengine yenye uhitaji huo.

"Kwa niaba ya Hospitali ya Muhimbili, tunawashukuru sana kwa msaada huu wa vifaa mliotupatia utakwenda kusaidia kuongeza ufanisi kwenye huduma zetu na tunaahidi tutavitunza," alisema.

Kiongozi wa timu ya msafara wa madaktari hao, Meng Yong, alisema Tanzania na China zimekuwa zikishirikiana katika sekta ya afya na wameamua kutoa msaada huo ili uweze kusaidia huduma zinaozotolewa Hospitali ya Muhimbili.

Alisema timu yake yenye wataalamu kwenye maeneo tofauti ya afya itakuwa nchini kwa miaka miwili ikitoka huduma kwa Watanzania.

"Baadhi ya vifaa vilivyopokewa ni mashine mbili za oksijeni, ventilator mbili aina ya SC-5 na Shangrila 510S, portable autoclaves (electric) na Shanghai Hutong," alisema.



Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Prof. Lawrence Museru (kushoto), akipokea msaada wa vifaa mbalimbali vya matibabu vyenye thamani ya Sh. milioni 139.9, kutoka kwa kiongozi wa timu ya madaktari Jimbo la Shangdong, nchini China, Meng Yong, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: ROMANA MALLYA**

# Jafo asimamisha uzalishaji ngozi sababu kero wananchi

Na Joseph Mwendapole

SERIKALI imesimamisha shughuli za uzalishaji kwenye Kiwanda cha Sintakwame Investiment kilichoko Kurasini, Dar es Salaam, kutokana na biashara yake ya ngozi kusababisha kero kwa wakazi wa maeneo ya jirani.

Agizo la kusimamishwa kwa shughuli hizo lilitolewa juzi Dar es Salaam na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, alipotembelea eneo hilo kusikiliza kero za wananchi.

Kiwanda hicho kinahifadhi bidhaa za ngozi katika ghala la Kurasini na wananchi wa eneo hilo wamelalamika kwamba ngozi hizo zinatoa harufu kali ambayo imesababisha waishi maisha ya mateso.

Jafo alisema shughuli za kiwanda hicho lazima zisimame hadi wamiliki watakaporekebisha mazingira ya utunzaji wa ngozi hizo na kisha kupata kibali kutoka kwa Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

"Ofisi yangu imepokea malalamiko kutoka kwa wananchi wa hapa kurasini kwamba kuna kiwanda kinahifadhi ngozi harufu inakuwa kali hata kuishi kwenye nyumba zao inakuwa shida sana...nimeshuhudia mwenyewe haya ni makazi ya watu na kweli harufu inawasumbua sana," alisema Waziri Jafo.

Jafo alisema kwa kuwa eneo hilo ni makazi ya watu kiwanda hicho kingeweza kufanya biashara nyingine yoyote kama nondo, sarufi au mbao lakini biashara ya ngozi imekuwa changamoto kwa wakazi hao.

Alisema wakati mwingine ngozi hizo zimekuwa zikifikishwa kwenye kiwanda hicho zikiwa mbichi hali ambayo husababisha usumbufu mkubwa kwa wakazi wanaozunguka maeneo ya kiwanda.

"Nashukuru Manispaa ya Temeke na NEMC wamekuwa wakifuatilia kwa karibu kero hii inaagiza shughuli hapa zisimame.

Kama ngozi zikija mkiwa mmeshaziweka kwenye mazingira mazuri sawa lakini ngozi mbichi hapana kuanzia leo msifanya hivi," alisema.

"Hizi ngozi ambazo mmeshazikausha na ziko tayari kwa kuuzwa nje mimi nawaruhusu muendelee kuzisafirisha lakini msiingize bidhaa zingine za ngozi mpaka mtakapopata cheti cha tathmini ya athari kwa mazingira kwa sababu NEMC ndio watawaambia kama kufanya biashara ya ngozi eneo hili inafaa au haifai," alisema Jafo.

Alisema Tanzania ina maeneo mengi mazuri yasiyo na makazi ya watu ambayo wenye viwanda wanaweza kwenda kuwekeza ili kuondoa mikwaruzano na wananchi inapotokea hali kama hiyo ya harufu kali.

"Maelekezo yaliyotolewa na wataalamu wetu mwendelee kuyafanyia kazi na hakikisheni ngozi mtakazoingiza kwenye kiwanda hiki hazisababishi usumbufu kwa wananchi na sitaki kusikia malalamiko tena kuhusu eneo hili," alisema Waziri Jafo.

# Moto wateketeza vitu ndani ya nyumba

Na Marco Maduhu, SHINYANGA

WATU wanane wamenusurika kifo baada ya nyumba ambayo wanaishi mtaa wa Mwinamila, Manispaa ya Shinyanga kuungua moto na kuteketeza vitu vyote vilivyokuwamo ndani.

Tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa 11:00 jioni katika mtaa huo lakini haukusababisha madhara yoyote kwa binadamu zaidi ya kuteketeza samani zote za ndani

Fred Paulo, ambaye ni mtoto katika nyumba hiyo, alisema ilipofika majira hayo, alitoka kwenda kununua vocha huku simu yake akiwa ameiacha kwenye chaji na aliporudi ndipo akaona moto ukiwaka.

Alisema moto huo ulianza kushika kwenye sofa, ndipo ikabidi akimbie kwenda kuzima umeme na kuanza kuomba msaada kwa wasamaria wema kuuzima moto huo na kufanikiwa huku ukiwa tayari umeshateketeza kila kitu ndani lakini nyumba yao ilisalimika.

"Nyumbani hapa tunaishi watu wanane wakiwamo na wapangaji na huu moto ulianza kuwaka kwenye chumba changu. Nashukuru Mungu nyumba haijateketea yote bali tumepoteza samani zote za ndani," alisema Paul.

Shuhuda wa tukio hilo, Oscar Kunze, alisema alikuwa amekaa jirani na nyumba hiyo akimsubiri mtu, lakini akasikia kelele nyumba inaungua moto, ndipo alipofika eneo la tukio na kuanza kusaidia kuuzima, huku watu wengine wakiendelea kwenda na kufanikiwa kuuzima.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Minamila, Rukia Athumani, aliwapongeza wananchi kwa kujitokeza kwa wingi na kuokoa nyumba hiyo isiteketee kwa moto, huku akilitupia lawama Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kuchelewa kufika eneo la tukio na moto huo kuzimwa na wananchi.

Alisema amesikitishwa na jeshi hilo kutopokea simu kwa wakati na baada ya kupata taarifa hawakwenda kwa haraka na na walipofika walikuwa wamepanda kwenye bodaboda bila ya kuwa na gari, hivyo kusababisha wananchi kutaka kuwashushia kichapo lakini alizuia tukio hilo.

Mkuu wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Wilaya ya Shinyanga, Stanley Luhwago, alikiri jeshi hilo kukabiliwa na upungufu wa magari na kubainisha kuwa wana gari moja la kuzimiamoto ambalo nalo kwa sasa ni bovu. Alitolea pia ufafanuzi sakata la askari wa jeshi hilo kunusurika kupigwa na wananchi alipofika eneo la tukio bila kuwa na gari la kuzimia moto na kwamba askari huyo alikuwa na wenzake wakitoa mafunzo kwa wananchi namna ya kukabiliana na majanga ya moto karibu na eneo la nyumba iliyoungua moto na walipotaa taarifa ilibidi afike hapo haraka ili kutoa msaada wa awali.

Luhwago alisema katika matukio ya moto hua kuna vitu vingi vya kuwahi kutoa msaada, ikiwamo namna ya kuokoa vitu au watu wasidhurike na moto, na ndiyo maana askari huyo aliwahi ili akatoe msaada wakati askari wengine wakifanya mawasiliano ya kupata gari la kuzimia moto kutoka Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) Kambi ya Kizumbi.

Aidha, alisema chanzo cha moto huo bado kinachunguzwa na kutoa wito kwa wananchi waendelee kushirikiana na jeshi hilo kuwapatia taarifa za majanga ya moto wakati wakiendelea na ukarabati wa gari lao, pamoja na kutumia magari ya zimamoto kutoka kwa washirika wao.

# Serikali yabainisha mikakati kuendeleza ubunifu zaidi

**Na Maulid Mmbaga**

SERIKALI imeahidi kusaidia kazi za ubunifu kufahamika kimataifa kwa kuratibu na kuwaonyesha fursa ziliko na kuwaunganisha wadau mbalimbali ili kuongezea uelewa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana katika mwendelezo wa maadhimisho ya Wiki ya Ubunifu yaliyofanyika jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Mindi Kasiga, aliwataka Watanzania kujitokeza kuchangamkia fursa hizo.

Wiki ya Ubunifu Tanzania 2022, imeandaliwa na Mradi wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDP) kupitia progrumu ya Funguo kwa kushirikiana na wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, (COSTECH) na wadau wa sekta ya mawasiliano ikiwemo Vodacom.

Pia alitoa wito kwa wabunifu pindi wanapokuwa na ubunifu wasijifiche na wasikae kimya badala yake waende kwenye taasisi husika kama Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) na kueleza mawazo yao kwa ajili ya kupatiwa msaada wa kuendelezwa endapo itaonekana kuwa unafaa.

"Kama mtu una wazo na wewe ni mtanzania kwa kweli hatutaki ukwame usikae nalo, tunataka kuona wabunifu wengi zaidi na bunifu nyingi zikiibuliwa, na ubunifu ndiyo raha yake kila siku kije kitu kipya tuweze kutumia vizuri.

"Kuna mambo yanajitokeza katika mazingira ya sasa kwenye upande wa utalii ambayo ni muhimu kuhusisha ubunifu, hatuwezi tukaendelea kutangaza utalii kwa njia zile zile za zamani, ndiyo maana mpaka saivi tunaona amezungumzwa sana Rais Samia Suluhu Hassan na 'promotion' ya 'Royal Tour' ambayo imeelezea kiundani vivutio vya utalii vya Tanzania lakini pia kama nchi ya kipekee kwenye utalii," alisema.

Aliongeza wiki hiyo ya ubunifu imesaidia kuwaongezea uelewa na maarifa kwamba wanawekaje ubunifu kwenye kuangalia njia mbadala ya kutangaza na kuvutia watanzania kwenda kwenye utalii wa Tanzania.

Pia alibainisha kuwa siku hiyo alishiriki katika uzinduzi wa tovuti ya Safari Wallet iliyobuniwa na mtanzania kwa ajili ya kuratibu safari mbalimbali za utalii na nyinginezo nchini, huku akiahidi kuwa watasaidia kuipeleka kimataifa kwa kuwa jukumu lao kubwa ni kutangaza utalii na kuvutia wawekezaji.

Mwanzilishi mwenza wa kampuni ya Safari Wallet, Iddy John, alisema wiki ya ubunifu imekuwa ni changizi kukuza teknolojia hasa kwa vijana nchini na imeweza kutoa mafunzo yaliyosaidia kuwaongezea uelewa watanzania juu ya masuala ya ubunifu.

"Vijana wanakuwa wanapelekwa sehemu mbalimbali na tunaweza kuingia katika hatua ya kuweza kufikiria kuleta suluhu zinazoweza kutatua matatizo ya sisi wenyewe ndani kwa ndani, hivyo Safari Wallet inamuwezesha mtanzania kusafiri safari yoyote anayotaka kwa kulipa kupitia tovuti hii," alisema John.





Mkurugenzi Mkuu wa kampuni ya kutengeneza viatu ya Barron, Jacqeline Kawishe (katikati), akionyesha viatu vinavyozalishwa na kampuni hiyo, wakati wa kongamano la Wiki ya Ubunifu iliyoratibiwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) na Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo (UNDP), kupitia programu yake ya Ubunifu Funguo, jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni maofisa mauzo wa Barron, Naila Salumu (kushoto) na Nadya Mahiza. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mahakama yataja tarehe hukumu kesi ya Mwijaku

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu inatarajia kutoa hukumu ya kesi inayomkabili msanii wa maigizo, Bulton Mwemba, maarufu Mwijaku, Mei 31, mwaka huu.

Mwijaku anakabiliwa na shtaka la kusambaza picha za utupu mtandaoni kinyume cha sheria.

Mahakama hiyo ilifikia uamuzi huo jana baada ya Mwijaku na mashahidi wake wawili kumaliza kutoa utetezi wao mbele Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rhoda Ngimilanga.

Baada ya Mahakama kusikiliza na kupitia ushahidi wa mashahidi watano wa Upande wa Jamhuri na vielelezo vinne, mshtakiwa (Mwijaku) alikutwa na kesi ya kujibu.

Baada ya kutolewa uamuzi huo, Mwijaku alidai mahakamani huko kuwa atakuwa na mashahidi wawili na atatoa utetezi wake kwa kiapo.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa alitenda kosa hilo katika tarehe tofauti kati ya Septemba 17 na Oktoba 10, 2019 jijini Da r es Salaam.

Ilidaiwa kuwa katika tarehe hizo, Mwijaku alisambaza picha za utupu akitumia kompyuta yake kupitia mtandao wa WhatsApp.

# Mpiji Magoe kuondokana na kero ya maji

**Na Mwandishi Wetu**

WAKAZI wa Kata ya Mpiji Magoe mkoani Dar es Salaam, wanatarajia kuondokana na kero sugu ya maji, kutokana na mradi mkubwa wa maji unaotekelezwa kwenye eneo hilo, ambao utakamilika Mei, mwakani.

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kupitia mkoa wa kihuduma wa Kibamba, inatekeleza mradi wa kupeleka maji safi kwa wakazi wa eneo hilo ikiwa ni sehemu ya mradi wa maji Machimbo- Kilongo.

Akizungumzia utekelezaji wa mradi huo, Mhandisi Zainabu Mwangubo, ambaye ndiye msimamizi wa mradi, alisema mradi huo mdogo ulianza mwanzoni mwa mwezi huu na unatarajia kukamilika mwishoni mwa Mei, mwakani.

Mhandisi Mwangubo alisema mradi umehusisha kazi za ulazaji wa mabomba ya inchi 1.5 kwa umbali wa kilomita 2.8 na mpaka sasa kazi ya kuchimba na kulaza mabomba imekamilika kwa umbali wa kilomita 1.8 na kwamba kazi ya uchimbaji mitaro inaendelea.

"Mradi uko katika hatua nzuri ya utekelezaji na kazi inaendelea kwa eneo la mita 450 lililobaki na mafundi wako kazini kuhakikisha inakamilika ndani ya wakati ili wakazi wa eneo hili wapate huduma," alisema.

Mradi wa Machimbo - Kilongo unalenga kunufaisha zaidi ya wananchi 300 wanaoishi katika mitaa ya Vatican, Kilongo, Mwaseba na Torino katika Kata ya Mpiji Magoe.

Mjumbe wa Serikali ya Mtaa wa Mpiji Magoe, Michael Lusajo, aliishukuru DAWASA kwa kupeleka huduma ya maji katika mtaa wake na kuongeza kuwa tayari ameshakusanya fomu za wananchi 40 walio tayari kuunganishiwa maji.

"Naishukuru serikali ya awamu ya sita kupitia DAWASA kwa kutuletea huduma ya maji na ninaendelea kutoa wito kwa wananchi wa Mpiji Magoe maji yamefika, hivyo tujitokeze kuunganishiwa majumbani kwetu," alisisitiza Lusajo.

Naye mkazi wa mtaa wa Vatican, Caroline Mushi, aliishukuru DAWASA kwa kuwasogezea huduma ya maji kwa kuwa wamekuwa na changamoto kwa muda mrefu.

"Mradi huu ni neema kwetu, tunawashukuru sana DAWASA na tuna imani baada ya mradi kukamilika changamoto yetu itatatuliwa," alisema Mushi.

Mradi wa Machimbo-Kilongo ni moja ya miradi midogo inayotekelezwa na DAWASA ili kufikia azma ya serikali ya kuhakikisha wananchi wote wanapata huduma ya majisafi na salama ifikapo mwaka 2025.

# RC aagiza mwalimu ashushwe cheo chake

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Sophia Mjema, amemwagiza Katibu Tawala wa Mkoa huo, Zuwena Omari, kumwondoa katika nafasi ya ukuu wa shule, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Bulungwa, Daudi Kasanda, kwa kushindwa kutekeleza majukumu ya usimamizi wa miradi ya elimu shuleni.

Vilevile, amemwagiza Ofisa Elimu wa Mkoa huo kwa kushirikiana na Katibu Tawala kutafuta mwalimu mwingine ili kusimamia shule hiyo ambayo ina upungufu mwingi, ikiwamo kukatiwa huduma ya maji kwa kushindwa kulipa ankra za kila mwezi na kusababisha wanafunzi kutumia maji ya kisima ambayo siyo salama.

Dk. Mjema alitoa agizo hilo jana wakati alipofanya ziara yake ya kushtukiza katika shule hiyo na kukagua vyumba vinne vya madarasa vilivyojengwa kwa fedha za Uviko-19 huku akibaini uwepo wa madawati yasiyokidhi viwango ambayo yanatumiwa na wanafunzi.

Alisema serikali ilitoa Sh. milioni 80 katika shule hiyo kwa ajili ya ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa na samani zake za ndani na kubaini madawati 100 hayana ubora na kutoa siku 30 kwa kamati ya ujenzi kuyakarabati kwa fedha zao wenyewe.

Dk. Mjema alisema fedha hizo zinatokana na UVIKO-19 na zilitolewa, akiagiza: "Ukaguzi wa madawati ya vyumba vya madarasa yaliyojengwa kwa fedha za UVIKO-19 ufanyike mkoa mzima ili kujiridhisha kama samani hizo zinafaa kwa matumizi ila kwa madawati haya 100 ninatoa siku 30 kamati ya ujenzi iyakarabati kwa fedha zao wenyewe.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, aliahidi kuhakikisha madawati hayo yanafanyiwa ukarabati na kamati hiyo kwa wakati ili yatumike kwa wanafunzi na kuondoa tatizo la watoto kubanana katika dawati moja ilhali madawati yapo.

Mmoja wa wakazi wa Kata ya Bulungwa katika Halmashauri ya Ushetu, Abdallah Matungu, aliiomba serikali kumwajibisha mwalimu huyo.

Mkazi mwingine, Agnes John, alisema serikali inahitaji ukaguzi wa mara kwa mara katika miradi ya elimu inayoendelea katika shule za msingi na sekondari na inapobainika kuwapo kwa viashiria vya ubadhirifu walimu wakuu na kamati za ujenzi wawajibike kisheria.

# Kagera kinara mauaji, ubakaji

**Na Daniel Limbe,** BIHARAMURO

JESHI la Polisi limesema Mkoa wa Kagera unaongoza kwa makosa ya mauaji na ubakaji kwa kipindi cha miezi mitatu iliyopita hali inayosababisha wananchi kuishi kwa hofu.

Kamishna wa Ushirikishwaji Jamii kutoka Makao Makuu ya Polisi, Dk. Mussa Ali Mussa aliyasema hayo jana alipozungumza na madiwani, watendaji wa kata na vijiji huku akiwataka kukemea vitendo hivyo ambavyo vinafedhehesha mkoa huo.

"Kwa taarifa nilizonazo kwa kipindi cha miezi mitatu katika Mkoa wa Kagera inaonyesha siyo chini ya makosa 30 ya mauaji yametokea," alisema.

Dk. Mussa alisema ili kukabiliana na vitendo hivyo, viongozi wa wilaya, kata,vijiji, vitongoji na wananchi hawana budi kushirikiana na askari polisi waliopelekwa kila kata kwa kutoa taarifa za uhalifu na wahalifu.

"Lazima tuambizane ukweli, bila ushirikiano wa wananchi uhalifu hauwezi kuisha nchini. Kwa hiyo, madiwani ninawaomba sana ajenda ya ulinzi na usalama ipeni kipaumbele kwenye vikao vyenu na muanze kuitengea bajeti badala ya kujikita kwenye miradi ya maendeleo pekee," alisema.

Kwa mujibu wa taarifa za jeshi hilo, uhalifu ndani ya Mkoa wa Kagera umekuwa ukijirudia mara kwa mara, hivyo kuna haja kuimarishwa vikundi vya ulinzi shirikishi kila kitongoji, hatua itakayosaidia kuzuia badala ya kujikita kupambana na uhalifu huo.

Kamishna Mwandamizi wa Jeshi la Polisi, Engelbert Kiondo, aliwataka madiwani na watendaji wa kata kuacha imani za kutegemea kuwa jeshi hilo ndilo lenye jukumu la kumaliza uhalifu nchini, badala yake watambue kuwa wao ni walinzi wa amani kwenye kata zao.

Alisema suala la kuwapo kundi la vijana wanaojiita panya road limesababishwa na malezi na makuzi mabovu ya wazazi na umefika wakati wa kushirikiana pamoja ili kuondoa hali hiyo.

"Tatizo la panya road siyo la kunyoosheana vidole, ni jukumu letu sote kuimarisha malezi na makuzi ya watoto wetu," alisema Kiondo.

Baadhi ya wakazi wa mkoa huo waliozungumza na Nipashe, walisema kuwapo kwa mapori mengi kwenye mkoa huo ni sababu mojawapo ya wahalifu kujificha huko na kufanya matendo mabaya kwa jamii.

Mbali na kupongeza mpango wa polisi jamii, Diwani wa Biharamulo Mjini, David Mwenenkudwa, aliwasihi madiwani wenzake kuimarisha uhusiano na jeshi hilo ikiwa ni pamoja na kuandaa mazingira mazuri ya kuishi askari kata sambamba na ujenzi wa vituo vidogo vya polisi.




Mkuu wa Idara ya Masoko na Mawasiliano wa Benki ya Exim Tanzania, Stanley Kafu, akizungumza wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Msalaba Mwekundu Duniani na miaka 60 ya Shirika la Msalaba Mwekundu Tanzania (TRCS), yaliyodhaminiwa na benki hiyo, na kuambatana na zoezi la upandaji wa miti katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma mwishoni mwa wiki. Wengine ni pamoja na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo (wanne kulia) na (watano kulia) ni Rais wa TRCS, David Kihenzile. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Benki ya Exim yaahidi uwekezaji utunzaji mazingira

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

BENKI ya Exim Tanzania imeahidi kushirikiana zaidi na wadau na kuunga mkono juhudi za serikali katika kupambana na mabadiliko ya tabianchi kwa kushiriki kikamilifu katika jitihada za utunzaji mazingira hususani kwa upandaji wa miti.

Ahadi ya benki hiyo ilitolewa na Mkuu wa Idara ya Masoko na Mawasiliano wa Benki hiyo, Stanley Kafu, katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Msalaba Mwekundu Duniani yaliyokwenda sambamba na maadhimisho ya miaka 60 ya Shirika la Msalaba Mwekundu Tanzania (TRCS) yaliyoambatana na upandaji wa miti katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma mwishoni mwa wiki.

Akizungumza kwenye maadhimisho hayo yaliyoongozwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira, Dk. Seleman Jafo, Kafu alisema kupitia programu za benki hiyo zijulikanayo kama Exim Go Green Initiative na Exim Cares, benki hiyo imekuwa ikijihusisha na mikakati mbalimbali ya kijamii ikiwamo uchangiaji damu na utunzaji mazingira kupitia matawi yake yaliyo katika maeneo mbalimbali nchini.

"Kwa upande wa ukanda huu wa kati, Jiji hili la Dodoma limebahatika kuwa chaguo la Benki ya Exim katika kuendesha programu hii. Ni kipindi kama hiki mnamo mwaka jana, tukiongozwa na Waziri Mkuu mstaafu, Mheshimiwa Mizengo Pinda, tulishirikiana na wadau wengine mkoani hapa katika kupanda takribani miti 10,000 katika Kata ya Zuzu iliyoko hapa jijini Dodoma," alisema Kafu.

Mbali na kushiriki kikamilifu katika upandaji miti, benki hiyo pia ilichangia Sh. milioni 15 kwa TRCS ili kufanikisha upandaji miti.

Alisema taasisi za kifedha nchini, ikiwamo benki hiyo, zimekuwa zikiguswa na athari za kiuchumi zinazotokana na kuzorota kwa sekta za uzalishaji, ikiwamo kilimo, kutokana na mabadiliko ya tabianchi na hiyo imekuwa moja ya sababu kubwa zinazosababisha taasisi hiyo kuwa mstari wa mbele katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kutunza mazingira.

Akizungumza kwenye maadhimisho hayo, Waziri Jafo pamoja na kuipongeza benki hiyo pamoja na wadau wengine kwa kuunga mkono jitihada za utunzaji wa mazingira nchini, aliwataka Watanzania kuungana katika kujitolea utoaji wa huduma za jamii ikiwamo ushiriki wa uokoaji nyakati za majanga pamoja na ushiriki wa utunzaji wa mazingira kwa upandaji wa miti.

Rais wa TRCS, David Kihenzile, aliiomba serikali na wadau mbalimbali nchini kuendelea kuunga mkono jitihada za shirika hilo kwa kuwa zinalenga kuisaidia jamii moja kwa moja katika masuala mbalimbali ikiwamo majanga na dharura.

"Ndiyo maana tumeguswa sana na uungwaji mkono tulioupata kutoka kwa wadau mbalimbali ikiwamo Benki ya Exim kwa kuwa msaada wao umetuwezesha kufanikisha upandaji miti na uchangiaji damu.

"Tunawashukuru sana, tunaomba na wengine waige mfano huo kwa kuwa bado tunahitaji sana uungwaji mkono," alisema Kihenzile ambaye pia ni Mbunge wa Bunge la Tanzania.

# Utaratibu kupata nguzo bora za umeme waja

SERIKALI imeweka utaratibu mpya wa kupata nguzo za umeme nchini ambazo zitakidhi ubora unaohitajika.

Waziri wa Nishati, January Makamba, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Nyasa (CCM), Stella Manyanya.

Katika swali lake, Manyanya alitaka kujua serikali ina mpango gani wa kuwachukulia hatua ya kuwafukuza wanaotengeneza nguzo za umeme zisizo na ubora ambazo zinaharibika na kuoza haraka.

Akijibu swali hilo, Waziri Makamba alisema wiki kadhaa zilizopita alikuwa Mafinga kuzungumza na wadau wa nguzo nchini na walizungumzia suala hilo la uhakika wa kupata nguzo zenye ubora.

"Ni kweli kwenye maeneo mengi nguzo zilizoko hazikidhi ubora. Tumeweka utaratibu mpya wa kupata nguzo nchini lakini ubora unaanzia viwandani na vitakuwa chini ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS)," alisema.

Naye Mbunge wa Babati Vijijini (CCM), Daniel Sillo, alitaka kujua kama serikali itakamilisha mpango wa kusambaza umeme vijiji kwa muda iliyopanga kutokana na kero mbalimbali zinazosababisha kuwapo na kasi ndogo ya watu kupata huduma hiyo.

Akijibu swali hilo, Waziri Makamba alikiri kuwapo kwa tatizo la bei na upatikanaji wa vifaa vya umeme katika usambazaji wa umeme.

"Katika makubaliano mapya na mkandarasi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na mikakati tuliyojiwekea naamini ratiba ya kazi itakuwa palepale, nia yetu ni kukamilisha miradi hii kabla ya Desemba mwaka huu," alisema.

Alisema katika mkutano huo wa saba wa Bunge unaoendelea mameneja na wakuu wote wa REA nchi nzima wako Dodoma na watakuwa tayari kupokea hoja zote za wabunge kuhusiana na suala hilo la kuunganishiwa kwa umeme vijijini.

Kadhalika, alisema serikali imeamua kuajiri waratibu wa REA kila jimbo kutokana na vikwazo na maswali mengi kuhusu miradi ya REA.

Alisisitiza kuwa pamoja na vikwazo vilivyojitokeza katika usambazaji wa umeme vijijini ikiwamo suala la bei na upatikanaji wa vifaa, usambazaji umeme katika vijiji vyote nchini utakamilika mwishoni mwa mwaka huu kama ilivyopangwa.



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula (kushoto), akijadiliana jambo na Naibu wake, Ridhiwani Kikwete, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Shule, vituo vya afya kufikiwa huduma maji

WIZARA ya Maji inaendelea kubainisha shule na vituo vya afya vyenye tatizo la huduma ya maji na kazi hiyo itakakamilika mwezi ujao, Bunge lilielezwa jana mjini hapo.

Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, aliyasema hayo jana alipokuwa akijibu swali la msingi la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Neema Lugangira, aliyetaka kujua serikali imejipangaje kuhakikisha shule zote nchini zinapata majisafi na salama.

Katika swali lake la nyongeza, mbunge huyo alisema mkoa wa Kagera una shule za msingi 459 lakini shule katika halmashauri za Missenyi, Ngara, Biharamulo na Bukoba hazijaunganishwa na majisafi na salama.

"Je, serikali itanihakikishia shule hizi zitaunganishiwa maji ili kuokoa hatari ya zaidi ya watoto 400,000 wa shule hizi?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Mahundi alisema baada ya kubaini shule na vituo hivyo, kuanzia mwaka 2022/23, serikali itatekeleza mpango maalumu wa miaka mitatu wa kupeleka huduma ya maji kwenye taasisi hizo.

"Mpango wa serikali ni kuhakikisha huduma ya majisafi, salama na yenye kutosheleza inapatikana kwenye shule na vituo vya afya kote nchini. Hili ni agizo wizara imetoa kwa watendaji wote mikoani, nitarajie mabadiliko makubwa kwa shule zote Kagera.

Dhamira ya Rais (Samia Suluhu Hassan) ni kuhakikisha watu wote wanafikiwa na majisafi na salama ya kutosha, jitihada zinafanyika mwaka huu na hata mwaka ujao wa fedha," alisisitiza.




**Habari zote na Augusta Njoji**

# Serikali kusajili shule shikizi zilizokamilika

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imesema iko tayari kusajili shule zote shikizi zilizokamilika na kumaliza taratibu zote za usajili ili zianze kutoa huduma.

Naibu Waziri wa Ofisi hiyo, David Silinde, alibainisha hayo jana bungeni alipokuwa akijibu maswali la Mbunge wa Kiteto (CCM), Edward Kisau.

Katika swali lake, mbunge huyo alitaka kujua kauli ya serikali juu ya kusajili na kuboresha miundombinu ya shule shikizi zilizojengwa kwa nguvu ya wananchi.

Aidha, katika swali lake la nyongeza lililoulizwa kwa niaba yake na Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Asia Hamlaga, alisema serikali ilijenga shule shikizi 57 katika Jimbo la Kiteto na kuhoji lini serikali itaharakisha usajili wa shule hizo.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri Silinde alisema serikali iko tayari kusajili shule zote zilizokamilika, cha msingi tu zifuate taratibu zote zilizowekwa.

"Vituo shikizi ni vituo vilivyojengwa kwenye maeneo ambayo hayana shule au shule ziko umbali mrefu kutoka kwenye maeneo wanayoishi wananchi, vituo hivi kabla ya kusajiliwa kuwa shule kamili, hufanyiwa ukaguzi na ufuatiliaji na wadhibiti ubora wa shule kwa kushirikiana na maofisa kutoka ofisi za wakurugenzi watendaji wa halmashauri," alisema.

Pia alisema kama hakuna upungufu, taarifa ya ukaguzi pamoja na barua ya kuomba usajili hutumwa kwa Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ili shule husika ipate usajili.

"Ili vituo shikizi visajiliwe na kuwa shule, halmashauri pamoja na wananchi wa vijiji husika wayafanyie kazi maelekezo ya wadhibiti ubora wa shule ili shule hizo zipata usajili," alisema.

ama
ALHAMISI MEI 12, 2022
AFYA NA MAZINGIRA




**KIKIWEKWA KANDO KINYAA... Fahamu kinyesi na mkojo wake binadamu bado hazina endelevu**




**AFYA YA AKILI Unajua undani wa 'Panya Road' imo katika malezi ya ubongo wa mtoto?**

# Mtu anapougua maradhi akili, vyanzo na shida zake hizi hapa

**Na Mwandishi Wetu**

MAANDIKO ya kitabu cha Kituo cha Afya cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kinatamka magonjwa ya akili yanatajwa ni matatizo ya ubongo yanayomfanya mtu kuwa na hisia, fikra na matendo tofauti na yale yanayotarajiwa na jamii, hata wakashindwa kukabiliana na magumu ya maisha.

Magonjwa ya akili yanatajwa yanaweza kusababishwa na sababu ama za kibaiolojia au kisaikolojia.



Mtu anayehisiwa kuwa na maradhi ya akili. **PICHA: MAKTABA.**

**KIBAILOJIA & KISAIKOLOJIA**

KibaioIojia: Inatajwa kuchangiwa na kurithi vinasaba vya kibaiolojia kutoka kwa wazazi, huku kukiwapo sababu nyinginezo; matumizi ya dawa za kulevya na zao la magonjwa ya muda mrefu kama vile Ukimwi, degedege na malaria

Hapo kunatajwa mazao ya majanga, ubakaji, uvamizi, ajali, utekaji nyara, kukosa elimu na kukosekana ajira.

Pia, katika orodha hiyo kuna watu wanaofiwa, kutengana, talaka, ugoni, kufungwa, kufukuzwa kazi, kukosa mishahara, kustaafu kazi, kutokufanya vizuri kwenye masomo na kufukuzwa masomoni iwe chuo au shuleni.

Kisaikolojia:Kuna ufafanuzi kwamba ni matatizo yanayowaathiri watoto kimantiki katika mambo kama vile kunyanyaswa kingono, kupigwa na kutengwa, kutothaminiwa na kutokupatiwa matunzo stahiki.

**DALILI ZA UGONJWA**

Magonjwa ya akili yapo ya aina nyingi na dalili zake zinatofautiana kati ya moja na nyingine.

Dalili Kihisia; hapo mhusika kuna wakati anasikia sauti ambazo watu wengine hawazisikii, vivyo hivyo mtu anaona vitu ambavyo wengine hawavioni.

Sambamba na hilo, mtu anahisi anafuatiliwa na wengine wapo wanaokuwa na wivu uliopitiliza;kuna wenye kuhisi mawazo yao yanajulikana kwa wengine au yanazungumzwa kwenye vyombo vya habari.

Ishara nyingine inatajwa kuwa ni kuhisi kuwa mtu anatumia mawazo yake kufanya mambo ya namna fulani; kufikiwa harufu ambayo wengine hawaisikii; hisia za maisha hayana thamani na kuona bora kufa kuliko kuishi.

**DALILI MWILINI**

Hapo ni kwamba mtu ama anakosa furaha au kuwa na furaha kupita kiasi; wengine wanakuwa na wasiwasi au woga uliopitiliza.

Wapo wanaopoteza hulka ya kuongea, wengine wanaongea kupita kiasi; kuwa na hasira za haraka kufikia hatua ya kudhuru watu au kuharibu vitu; au kuwapo wanaotawaliwa na msongo wa mawazo; pia, hujitenga na watu, wakipenda kukaa binafsi muda mrefu.

Jingine linalotawala muda mrefu ni kutokuwapo ari ya kufanya kazi, au kufanya kazi nyingi kwa wakati mmoja, pasipo kuzikamilisha; kutoonyesha hisia usoni iwe furaha au huzuni; na kutojali usafi na mwonekano binafsi.

Pia, uangalizi huo unadokeza suala la mwili kukosa nguvu au kuhisi kuwa na nguvu za ziada; kukosa usingizi au kulala kupita kiasi; mtu kukosa hamu ya kula au ulaji kupita kiasi; kutotulia, pia kuwa na hisia za kuhamanika au kutulia sehemu moja muda mrefu bila ya kujisogeza

Sambamba na hali hiyo, kuna mtazamo wa mwili wa mtu kuwa na maumivu ya sehemu mbalimbali, huku hospitalini vipimo havionyeshi tatizo lolote.

**DALILI ZA KIAKILI**

Ni orodha inayojumuisha kukosekana umakini kwenye shughuli binafsi za kila siku; kusahau kwa haraka au kupoteza kumbukumbu; kukosa uwezo wa kupambanua mambo kwa mitazamo tofauti; akijiamini ni mtu maarufu au nabii.

Mingine inajumuisha imani zisizo za kawaida kama vile kupokea taarifa redioni au kwenye mitandao ya simu; imani ya kuwasiliana na watu

maarufu, kujihisi kuwa na nguvu ya ziada nje ya mwili wake; akijihisi watu wanamfuatilia kumdhuru; na mawazo yake hukosa mtiririko unaoeleweka.

**MATIBABU YAKE**

Matibabu ya magonjwa ya akili hutofautiana kati ya ugonjwa mmoja na mwingine. Hapo inahimizwa elimu kwa jamii kuhusiana na magonjwa ya akili, cha muhimu kusisitizwa ni kuepuka isijirudie, juu ya matibabu na mhusika awezeshwe kuendelea na maisha yake ya kila siku.

Masuala kama vile kufanyiwa uchunguzi mapema

ili apatiwe tiba sahihi na ya mapema, pia tiba ya kisaikolojia inayomuwezesha kujitambua aliko, anapotaka kuwa, hata akafanya mabadiliko kwa kutegemea uwezo wake mwenyewe.

Tiba kimwili ni kwa kutumia dawa za hospitali matibabu kwenye nyumba za upataji nafuu (Sober Houses); ushirikiano kati ya mgonjwa, familia na wataalamu tiba ukitajwa ni mzizi wa mafanikio makubwa katika matibabu.

Ipo sura nyingine inayojumuisha kutotumiwa dawa za kulevya; kuwa na muda wa kutosha kupumzika;

kufanya mazoezi; kujitenga na jamii; hali kadhalika kujibidiisha na shughuli za kuleta kipato.

• ***Soma makala zaidi ukurasa 12.***

AFYA

ILIVYO AFYA YA AKILI NA NYENDO ZAKE

# Unajua undani wa 'Panya Road' imo katika malezi ya ubongo wa mtoto?

• Nafasi ya wazazi iko nyuma ya pazia

Na Pankras Luoga, MUHAS



Ndivyo hali ilivyokuwa kwa watuhumiwa wa 'Panya Road'. **PICHA: MTANDAO.**

MAANA halisi ya mitaala ya matatizo au maradhi ya ubongo ni hali inayomfanya mtu kuwa na hisia, fikra na matendo tofauti na yanayotarajiwa na jamii, hata kushindwa kukabiliana na shida za kimaisha.

Hapo inaangukia dhana afya ya akili, hata matokeo yanayozalishwa na mageuzi hayo ni utofauti wa tabia binafsi au kikundi cha vijana. Hapo ndipo kunapozuka tafsiri au dhana 'afya ya akili' inayoendana moja kwa moja na za mtu au kikundi.

Katika zao la dhana au tabia hiyo, ndiyo inakoibua kikundi cha vijana ambao baadhi wana mwenendo usiokubalika kijamii, ukibeba mantiki za kihalifu zenye jina 'Panya Road' hata kuibua kauli ya mkuu wa nchi, Rais Samia Suluhu Hassan, anayekemea, sambamba na Mkuu wa Jeshi la Polisi, Simon Sirro.

Wazauoni wataalamu, wakiwamo kwenye andiko la Kituo cha Afya cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wanafafanua mzizi husika wa tabia aina hiyo, iwe kibaiolojia au kisaikolojia, inajumuisha na sababu; kutofanya vizuri masomo au kufukuzwa, kupigwa na kutengwa, kutothaminiwa na kutokupatiwa matunzo stahiki.

**INAKOANZIA & NAFASI YA WAZAZI**

Kimsingi 'Panya Road' ni kikundi cha kihalifu kinachoundwa na vijana wa umri tofauti, wengi wao wakiwa na umri chini ya miaka 20, wakijihusisha na uhalifu wa kupora mali na kujeruhi usiku wa manane.

Ni aina ya vikundi vinavyojitokeza kwa muda fulani na kisha wanapotea, baada ya kutekeleza vitendo hivyo vya uhalifu. Hivi karibuni, wamejitokeza katika maeneo mbalimbali ya jiji la Dar es Salaam, ikiwa ni pamoja na Mbagala, Chanika, Tabata na Mtongani- Kunduchi.

Mara zote, wanakikundi wakiwa katika jumuiya chini ya uangalizi kabla ya kujitegemea, wazazi na walezi ndiyo wa kwanza kabisa katika jukumu la kudhibiti uhalifu au tabia hiyo hasi, kwa sababu ndiyo waliowazaa, kuwakuza na kutoa mfano wao kuishi na wanawajua vizuri watoto hao.

Mtazamo wa kimantiki hata kupotoka wakafikia saikolojia hiyo mbaya yenye madhara kwa watoto hao, wazazi na walezi husika katika jamii wanahusika na ufuatiliaji usioridhisha kitabia kwa watoto, kufikia madhila hayo.

Kidole kimojawapo kinachonyooshwa ni zao la kubadilika mifumo ya maisha, ikiwa ni pamoja na wazazi na walezi kuzama zaidi katika majukumu ya kutafuta pesa na mahitaji kwa ajili ya familia, kipaumbele cha kusimamia tabia na mwenendo kuwa na nafasi ndogo.

Hiyo inatajwa kutokana na kushamiri na kuenea utandawazi, hasa matumizi ya simu na mifumo yake ya mitandao ya kijamii kama "whatsapp" hata wakatumia muda mfupi sana kukaa, kuongea na kujua tabia za watoto kwa undani, marafiki na makundi wanayochangamana nayo.

Kushindwa huko kutathmini na kufuatilia kwa karibu watoto, kunatoa nafasi kwa watoto hao kubadilika kitabia kuelekea kwenye mabaya na hata kunashuhudiwa kujihusisha na mabaya, ikiwamo ya makundi kama 'Panya Road' bila wazazi na walezi wakati mwingine hawatambui kinachoendelea.

Pia, ni ulingo unaotoa mwanya watoto wanatoka usiku wa manane kutekeleza vitendo hivyo vya kihalifu na uporaji, pasipo wazazi kujua, wakiamini wako nyumbani. Zao lake ni mambo kama; uhalifu wa kupora mali na kujeruhi watu, matumizi ya dawa za kulevya, wizi hata ujambazi.

**TIBA YA MSIMAMIZI**

Kwanza, wazazi na walezi wanatakiwa kujiweka sawa hata wakawa mfano wa kitabia kwa watoto wao, kikubwa kuimarisha tathmini na ufuatiliaji wa karibu wa watoto wao.

> **Hicho ni kitendo kinachowasaidia wazazi na walezi kujua maendeleo ya watoto wao kitabia, marafiki na makundi wanaoshirikiana nao na zao lake ni kupunguza kasoro katika malezi na tabia za watoto kama vile watoto kushiriki katika vikundi vya uhalifu mfano 'Panya Road.'**

Hicho ni kitendo kinachowasaidia wazazi na walezi kujua maendeleo ya watoto wao kitabia, marafiki na makundi wanaoshirikiana nao na zao lake ni kupunguza kasoro katika malezi na tabia za watoto kama vile watoto kushiriki katika vikundi vya uhalifu mfano 'Panya Road.'

Pia, inakuwa fursa kuwasaidia wazazi na walezi husika, kutambua mapema kasoro za kitabia kwa watoto wao, hata wakazitafutia ufumbuzi mapema kabla ya kushuhudiwa madhara ya jamii.

Kitaalamu, tathmini na ufuatiliaji wa karibu wa tabia za watoto, inalezwa ni lazima ianzie katika ngazi za familia na shuleni, kwa kushirikiana na walimu shuleni na mamlaka za kidini.

Ukamilifu katika kufanya tathmini na ufuatiliaji wake wa karibu, unaweza kuwahusisha wazazi na walezi wakifuatilia mienendo ya watoto wao kujua mabadiliko ya tabia zao.

Hapo inatajwa walezi wanatakiwa kufuatilia ratiba sahihi kama inavyotakiwa na kuondoa uwezekano wa watoto wao kujiunga na makundi hasi kitabia, bila ya wazazi wao kujua.

Mfano hai ni kuwafuatilia kwa karibu watoto kila mara au baada ya muda fulani, kunasaidia kugundua kama wanaenda kulala au wanatoka usiku na kwenda kutekeleza uhalifu mitaani.

Cha msingi, ni kwa walezi na wazazi kutimiza jukumu hilo muhimu, wakizingatia misingi ya tathmini na ufuatiliaji, yaani wao wenyewe kuwa mfano wa tabia njema katika jamii, kutoa mahitaji husika kwa watoto na kuchua hatua mapema katika kuwarekebisha kasoro za kitabia, ili watoto hao wapevuke kimaadili na tabia njema katika jamii zao.

Hapo inajumuisha mzazi au mlezi kuhakikisha mtoto anapewa mahitaji yote muhimu, kama chakula, vifaa vya kujifunza, upendo, heshima, mavazi na hamasa juu ya tabia njema katika maisha yake na jamii kwa ujumla.

• ***Mwandishi ni Mhadhiri Msaidizi katika fani ya Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Afya, katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Tiba Muhimbili (MUHAS). Anapatikana kwa simu: +255 757- 645746.***

AFYA

# Shinyanga yasitisha kufuata huduma Bugando, ikipewa kifaa cha Uviko 19

## • Msaada wa wawekezaji mgodi dhahabu

**Na Shaban Njia, KAHAMA**



Msimamizi wa Kitengo cha Afya Mgodi wa Bulyanhulu Dk. Kudra Mfaume, akitoa maelezo ya matumizi ya mashine mbili za kupima Uviko-19, zilizotolewa na mgodi huo kwa Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk.Sophia Mjema. **PICHA; SHABAN NJIA**

NI miaka mitatu sasa tangu Tanzania itangaze mgonjwa wake wa kwanza wa virusi vya Covid-19, tangu tarehe 16, Machi mwaka 2020.

Kuna jitihada zilizofanywa na serikali kwa kushirikiana na wadau wa afya kutoa elimu kwa umma kuhusu mlipuko wa ugonjwa huo mpya corona, ambao dalili zake zilielezwa, pia namna yake kuepuka maambukizi.

Jamii ilielimishwa kunawa mikono, kutumia vitakasa mikono, kuepuka misongamano kwa kuzingatia umbali baina ya mtu mmoja na mwingine na kutumia barakoa kuzuia maambukizi ya kukohoa au chafya.

Hata hivyo, Tanzania haikufuata mkondo wa nchi nyingi wa kufunga mipaka na shughuli zote za kijamii, huku baadhi tu ya shughuli zilifungiwa kama michezo na mikusanyiko ya harusi na maeneo ya starehe kwa muda, baadaye zikafunguliwa.

Shughuli nyinginezo za kijamii, ziliendelea kama kawaida huku aliyekuwa Rais wa Tanzania wakati huo, Dk. John Magufuli akiwahimiza wananchi wake kuchapa kazi na kuondoa hofu huku wakichukua tahadhari ya kujikinga.

Magari ya kusafirisha abiria (daladala) yalipewa utaratibu wa kuingiza abiria na na watu kukaa bila kubanana,japo kulikuwapo na milolongo mirefu kuingia ndani ya magari hayo, hata ililеta heshima ya kutokuenea kwa kasi zaidi kama ilivyotabiriwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) kwamba watu wengi zaidi wangepoteza maisha.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Wizara ya Afya kuhusu mwenendo wa ugonjwa Uviko-19, hadi kufika Mei 4 mwaka huu, jumla ya watu 33,916 walithibitika kuwa na Uviko-19 na idadi ya vifo vilikuwapo 803.

Katika kipindi hicho, mkoa wa Dar es Salaam umeendelea kuongoza kuwa na idadi kubwa ya waliothibitika kuwa na ugonjwa huo; kuwapo matukio ya maambukizi mapya 70 sawa na asilimia 87.5 ya idadi yote ya wagonjwa.

Mikoa mingine iliyoambukizwa Uviko-19 ni Arusha (6), Kilimanjaro (2), Morogoro na Mwanza, kila moja iliripotiwa mkasa wa mtu mmoja.

Taarifa hiyo inasema, serikali imeendelea kutoa huduma za chanjo kote nchini ili kuwezesha wananchi kupata kinga dhidi ya ugonjwa huo, toka kuanza kuchanja jumla ya watu 3,999,988 sawa na asilimia 13.01 ya Watanzania 30,740,928 wenye umri zaidi ya miaka 18, walikuwa wameshapata dozi kamili ya Uviko-19.

Kwa kuona ukubwa wa ugonjwa wa Uviko-19 wadau wa maendeleo ikiwemo kampuni ya uchimbaji wa madini Barrick Bulyanhulu, imetoa vifaa vya kisasa vya kupima na kutoa majibu ya ugonjwa huo katika Hospitali ya Manispaa Kahama, ikiwa ni namna ya kusogeza huduma karibu.

Msimamizi wa Afya kutoka Bulyanhulu, Dk. Kudra Mfaume, anasema mgodi umekabidhi vifaa vya kisasa vya kupima virusi vya ugonjwa wa Uviko-19 katika Hospitali ya Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, vyenye thamani ya Sh. Milioni 115 kuhudumia wananchi wa wilaya jirani.

Dk. Saidi anafafanua, vifaa vilivyotolewa katika hospitali hiyo aina ya RT-PCR, mashine mbili zenye uwezo wa kupima sampuli nne ndani ya saa moja na kutoa majibu, hali anayoitaja itawaondolea wananchi adha kusafiri mpaka Hospitali ya Bugando jijini Mwanza, kupata vipimo hivyo.

"Tunaomba mashine hizi zitunzwe na kutumika katika matumizi yaliyopangwa, ili ziwasaidie wananchi wa wilaya hii na mikoa jirani, katika kuhakikisha zinafanya kazi kwa wakati na ufanisi. Tutaleta wataalamu wetu kwa ajili ya kuzifunga na kuzisajili na mifumo ya Wizara ya Afya," anaeleza Dk. Mfaume.

Pia, anataja lengo la utoaji mashine hizo ni mwendelezo wa kuunga mkono jitihada za serikali kupambana dhidi ya Uviko-19 hivyo mashine hizo zitakuwa msaada mkubwa kwa wananchi, kulinganisha na wilaya ya Kahama yenye mwingiliano wa watu wengi kutoka nchi jirani.

### WAGANGA WAANDAMIZI

Dk.Lucas David, ni Mganga Mkuu wa Hospitali ya Manispaa ya Kahama, anasema mashine hizo zitasaidia nguvu ya kuwahudumia wagonjwa, kwani mwaka 2019 walichukua sampuli za Uviko-19 na kuzisafirisha hadi Bugado, Mwanza kuipatia majibu.

Anasema, ni usafishaji uliochelewesha majibu kati ya wiki moja hadi mbili, hali iliyowaathiri sana waliotaka kusafiri walilazimika kuachwa na ndege na shughuli zao zililazimika kusimama mpaka majibu yalipotoka.

Dk. Lucas anasema, tangu kuingia ugonjwa huo jumla ya wagonjwa 387 waliugua na kulazwa, hivyo uwepo wa mashine hizo utasaidia kuboresha huduma na kwa wale watakaohitaji kusafiri haraka majibu, yao yatapatikana mapema, hata wasiathiri ratiba zao.

Mganga Mkuu wa Mkoa, Dk. Daniel Mzee anasema Shinyanga iliathirika kwa kiwango kikubwa na ugonjwa huo, hasa wimbi la tatu na akaahidi kuzitunza mashine hizo zitumike kama inavyopaswa, ili kuwanufaisha wananchi wote.

### MKUU WA MKOA

Akipokea vifaa hivyo Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga. Dk. Sophia Mjema, anasema vifaa hivyo vya upimaji wa ugonjwa wa Uviko-19 vitasaidia kupunguza maambukizi hasa katika wimbi hili la tatu, ambalo bado linaendelea kuuathiri umma.

Pia, anawataka wasimamizi wa hospitali hiyo kuwatangazia wananchi uwepo wa vifaa hivyo, ili wapate muda wa kuchunguzwa na kutambuliwa mapema afya zao.

Mjema, pia anawataka wataalamu wa afya waendelea kuwasisitiza wananchi katika maeneo yao kufuata sheria zote za kujikinga na ugonjwa huo, ikiwemo mikono na maji tiririka, kujitakasa mikono wakati wote na kuondokana na misongamano isiyokuwa na tija au lazima.

### WANANCHI & KLINIKI TEMBEZI

Mratibu wa Huduma za Tohara Manispaa Kahama, Dk.Hajji Swedi, katika uzinduzi wa huduma ya kliniki tembezi, anasema ni kawaida yao wanapofika katika maeneo yenye vijana balehe na wanaume wasiopata tohara, huwa wanaanza na elimu ya Uviko-19 wakiwakumbusha kujikinga.

Anaeleza, kliniki tembezi imewaamsha kujitokeza hadi wakapata chanjo ya Uviko-19 hospitalini na hiyo ni baada ya kuwafikia na kuwakumbusha uwepo wa maradhi hayo na umuhimu wa chanjo.

Mkazi wa Kata ya Nyahanga, Baraka John, anasema wamekuwa wakipata elimu kila mara namna ya kujikinga na corona, kupitia kliniki tembezi na amekuwa akichukua tahadhari kila anapokuwa kwenye msongamano wa watu, ikiwemo magulioni na minadani.

Mkazi mwingine, Samweli Godfrey, anasema huduma hiyo inasaidia kupunguza adha ya kutembea umbali mrefu kufikia vituo vya afya kupata huduma ya tohara na chanjo ya Uviko-19 na awali walikosa huduma ya tohara, baada ya kukuta msongamano wa wateja hospitalini na sasa wanapata kwa wakati.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk.Sophia Mjema akikata utepe kuashiria kuzinduliwa mashine mbili za kisasa za upimaji Uviko-19. Kushoto kwake ni Meneja wa Mgodi huo, Cheick Sangare na kulia kwake Meneja wa Mgodi wa Buzwagi, Rebecca Stephen. **PICHA: SHABAN NJIA**

MAZINGIRA

## KIKIWEKWA KANDO KINYAA...

# Fahamu kinyesi na mkojo wake binadamu bado hazina endelevu

## •Rekodi za kihistoria zinaendelea kutetea




Shughuli za utiririshaji majitaka ya vyoo zikiendeelea. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Na Mwandishi Wetu**

MAISHA ya binadamu, kama ilivyo kwa viumbe vingine ikijumuishwa na wanyama, wanalishwa na kisha yasiyohitajika, hutolewa kwa mfumo maalum wa kibaiolojia, zikiwa ni uchafu.

Ikirejewa hulka ya mwanadamu anachoingiza mwilini mlo hufurahia katika namna ya bashasha kuvutiwa na ladha, pia harufu, lakini mabaki yake yanapotolewa nje, huambatana na kinyaa, hata kwa kuziba pua kutopenda harufu hiyo mpya, hasa ikiwa sio cha mhusika.

Kuna sura kuu tatu ya vitokavyo kutoka mwili wa binadamu baada ya kutumiwa kama mlo; Inaanza na jasho, kisha mkojo na kinyesi, kila kimoja kikiwa na jia yake ya kutoka.

**MANUFAA YAKE**

Mara nyingi watu huziba pua zao kwa kuhisi harufu mbaya ikionekana haifai, hasa linapokuja suala la kinyesi na mkojo.

Lakini, katika sura ya pili uchafu huo kutoka mwilini, una manufaa ya kubeba matumizi makubwa. Kwa vipi? Kitalaamu kinyesi kina nguvu kubwa kiasi cha kuweza kuokoa maisha ya baadaye ya mwanadamu.

Aidha, kitaalamu mtu mzima anatoa kilo 91 za kinyesi na lita 730 za mkojo kila mwaka. Kurejea historia ya kutoka jijini Roma, Italia tangu zama zilizopita na dhana kuenea katika nchi nyingi, taka za binadamu kwa maana ya kinyesi na mkojo, hazikutupwa.

Majitaka ambayo hayajatibiwa, yalitumika kama mbolea kwenye bustani na wakati huohuo, mkojo ulitumiwa viwandani kutengenezea nguo.

Hapo ndipo kukazaa historia ya cheo kinachoitwa Mfanyakazi wa Usafi wa Mfalme, kikiwa mojawapo ya nyadhifa muhimu wakati wa Mfalme Henry wa Uingereza kati ya mwaka 1509 hadi 1547.

Mtu aliyekuwa anafanya kazi katika nafasi hiyo, akabeba jukumu la kusaidia usafi wa chooni kila siku na akaonekana mtu wa karibu sana na mfalme huyo wa Kiingereza.

Wakati huo kulikuwapo watu waliozoa taka hizo usiku na kuziuza kwa wakulima wa eneo hilo. Mkojo ulikusanywa na kutumika kulainisha ngozi, huku mfanyakazi wa usafi wa mfalme akawa ni mmojawapo ya wenye wadhifa muhimu wakati wa mfalme huyo.

**DUNIA INAKOELEKEA**

Kwa kurejea nadharia hiyo katika maisha ya sasa, inaelezwa ni inayofaa umma kujifunza kutoka kwa mababu kuhusu umuhimu wa kinyesi, wataalamu wakisema inaweza kutoa suluhisho kwa matatizo mengi ya sasa.

Ikianzia na shida ya nishati, inaaminika kuwa vitu vingi vyenye nyuzi nyuzi vinapaswa kuliwa ili kusafisha vizuri tumbo na haisababishi shida ya kuvimbiwa.

Hiyo inatajwa ni rasilimali ambayo usambazaji wake unaweza kudumishwa kila wakati. Katika hali hiyo, inaweza kuaminika zaidi, ikilinganishwa na ugavi unaoendelea wa maji, hewa au rasilimali nyinginezo kwenye uzalishaji nishati.

Tope linalobaki baada ya kusindika maji taka kinyesi kinaweza kutumika kama malighafi nzuri ya kutengeneza kemikali ya methane, ambayo ni wakala mkubwa wa kutoa gesi yenye uhusiano na joto.

Ni kawaida, hata katika mitambo ya kisasa ya matibabu, bakteria huchanganywa nayo kutengeneza gesi ya baiogesi inayopitishwa kwenye bomba hadi majumbani au kutumika kama mafuta kwenye magari.

Hayo yanatajwa kuwa mafuta safi zaidi kuliko petroli au dizeli. Hapo ndipo inapozaliwa hoja, kwamba kupata majitaka ya kinyesi na mkojo, kunaweza kuchangia kupunguza utegemezi wa umma kwenye petroli, dizeli na gesi.

Faida kubwa nyingine ni kwamba, inahesabiwa mahali hapo kutapunguzwa msukumo kwa maliasili zilizopo, pia kudhibiti uzalishaji hewa chafu ya kaboni katika mazingira.

**NAFASI YA MKOJO**

Mkojo unatajwa kuwa na manufaa kwa wanadamu, ikizingatiwa angalizo kwamba asilimia 72 ya maji yanayotumika duniani ni kwenye kilimo.



Katika siku zijazo, kunatajwa matarajio kwamba, kuna ongezeko la idadi ya watu na mabadiliko ya hali ya hewa, vitakavyoongeza zaidi mahitaji ya maji.

Dira ni kwamba, katika miaka 10 zijazo, kunaweza kuwapo hali kama hiyo katika nchi zingine na sababu za ukosefu wa maji hata watu wakalazimika kuondoka mahali waliko.

Zipo takwimu za nchini Uingereza, kwamba watu hutoa lita mbili za mkojo kila siku na anatumia lita 140 za maji kwenye shughuli mbalimbali za nyumbani.

Kuna suala la kuchakata mkojo linaloelezwa lina nafasi ya kuokoa dunia na hatari ya ukame. Ni teknolojia inayopatikana pia na tayari inatumika.

Katika kinachofanana na hicho, nchini Israel kwa sasa kumeshazalishwa mabwawa 56,000 ya maji ya michezo ya kuogelea na yatakayotumika, yanachakatwa kwa ajili ya kutumika shambani.

**MATUMIZI YA TAKA**

Inaporejewa kilimo, ukizungumzia kilimo, kitu chochote kilicho hai kinategemea madini fosforasi ili kiweze kuishi. Hata hivyo, kutokana na uchimbaji madini kupita kiasi, inapungua kwa kasi na haiwezi kujazwa tena.

Nchi za Amerika, China na India zinatajwa huenda zikakabiliwa na upungufu wake katika vizazi vyao vijavyo, huku ikijulikana hata kilimo shambani bila ya kuwa na fosforasi ya kutosha, uzalishaji unaweza kutoa nusu tu ya mavuno.

Wazee zamani walitumia taka katika udongo kama vile kutumia mabaki makavu yenye virutubisho vingi yaliyoachwa kutoka vyooni, wakatengeneza mboji au katika kuzalisha gesi asilia.

**MABADILIKO CHOONI**

Suala la kujengwa upya vyoo, kunatajwa kunaweza kuleta mabadiliko makubwa kutokana na kuwapo watu bilioni nne na milioni 200, wasiokuwa na njia safi ya kujisaidia, vyoo visivyo na maji ya bomba wakiambatana na kuokoa hatari ya vifo kwa jumla ya watoto takriban 800 wenye umri chini ya miaka mitano.

Bill Gates, Mwanzilishi Mwenza wa kampuni ya kimataifa ya Microsoft, aliwahi kusema kuwa soko la vyoo linakua sio tu kuokoa maisha, bali pia lina manufaa mbalimbali na mtazamo wa biashara.

Anafafanua matarajio yaliyoko ni kwamba, ifikapo mwaka 2030, soko la vyoo litafika Dola za Marekani bilioni sita (wastani Sh. Trilioni 13.94).

Biashara ya kuuzwa bidhaa ya choo yenye thamani ya Dola moja au Sh. 2,323 itazalisha Dola tano au sawa na Sh.11, 615.

• ***Kwa mujibu wa BBC.***



# Askari Zimamoto waonywa rushwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

NAIBU Katibu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Ramadhani Kailima, ameonya kitendo cha baadhi ya askari, maofisa na wakaguzi wa Jeshi la Zimamoto na Ukoaji, kuhusu kujihusisha na rushwa katika utekelezaji wa majukumu yao.

Kailima aliyasema hayo jana wakati wa ufunguzi wa Baraza la Wafanyakazi wa Jeshi hilo uliofanyia jijini Dodoma.

Alisema ni kosa kwa mtumishi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kutuhumiwa kwa rushwa, ikiwamo kunyooshewa vidole na wananchi, hivyo kama kuna mtu anafanya hivyo, anapaswa kuacha mara moja.

Suala la rushwa, alisema ni kilio kikubwa kwenye sekta ya umma, hivyo ni vyema kuepuka kunyooshewa vidole na wananchi badala yake wafanye kazi kwa bidii kama sheria inavyoelekeza.

Pia alisema katika utekelezaji wa majukumu ya jeshi, ni hatari kwa ofisa, mkaguzi au askari kuchukua rushwa na kwamba kufanya hivyo maana yake anahalalisha kutokea kwa moto na majanga mengine.

Kailima alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kutokana na kuleta mabadiliko ndani ya mwaka mmoja wa utendaji kazi na kwamba moja ya mabadiliko hayo ni Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, ambayo yanaliwezesha jeshi hilo kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Aliainisha kuwa katika kipindi cha mwaka mmoja, maofisa na wakaguzi wa Jeshi la Zimamoto na Ukoaji 149 wamepandishwa vyeo, vikiwamo kupewa kibali cha kuajiri askari wapya 400 ambao kwa sasa wako mafunzoni pamoja na maofisa, wakaguzi na askari 918 kuhudhuria mafunzo.

Akitoa maelezo mafupi ya baraza kwa niaba ya Mwenyekiti wa Baraza hilo, Baraka Semwanza ambaye ni Kamishna wa Utawala na Fedha, alisema wamefanya shughuli mbalimbali za uokozi kwa kuyakabili matukio ya moto 1,226.

Kwa upande wa uokozi, Kamishna Semwanza alisema kulikuwa na matukio 455, vifo 370 na majeruhi 826.

Hata hivyo, alisema bado jeshi hilo linakabiliwa na uhaba wa nyumba za watumishi na ofisi katika mikoa na wilaya mbalimbali nchini.

# Wapongeza Ndugai kutangaza kustaafu

**Paul Mabeja,** DODOMA

BAADA ya aliyekuwa Spika wa Bunge, Job Ndugai, kutangaza kutogombea tena ubunge Jimbo la Kongwa katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025, wadau mbalimbali wametoa maoni yao huku wengi wao wakimpongeza kwa uamuzi wake.

Kada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) jijini Dodoma, Bashiru Kajuna, alisema kwa kiongozi wa siasa kuachia nafasi yake kwa hiari ni jambo la kupongezwa kwa kuwa wengi wamekuwa wagumu kuachia madaraka hata kama wananchi wamewachoka.

"Mimi nimpongeze sana Ndugai. Ni vigumu sana kwa wanasiasa kutangaza kuachia madaraka kirahisi kama hivi. Nampongeza sana na wengine wanapaswa kuiga badala ya kung'ang'ania madaraka hadi kuondolewa katika nafasi zao kwa aibu.

"Kati ya viongozi ambao nimewaona katika maisha yangu ni wachache ambao wameachia nafasi zao kwa hiari akiwamo Baba wa Taifa, Mwalimu Julias Kambarage Nyerere," alisema.

Mbunge wa Bahi, Kenneth Nolo, alisema anampongeza Ndugai kwa kuamua kustaafu kwa heshima kutokana na kuwatumikia wananchi wa Kongwa kwa zaidi ya miaka 20.

"Mimi kama ambavyo wengine wamesema, nampongeza sana Ndugai kwa uamuzi wake na wengine tunapaswa kuiga kustaafu kwa heshima," alisema Nolo.

Mbunge wa Mvumi, Livingston Lusinde, alisema anamtakia kila la heri Ndugai na anatoa wito kwa wanasiasa ambao wametumikia nafasi zao kwa muda mrefu kuiga mfano huo kwa kung'atuka badala ya kusubiri kuondolewa kwa aibu.

Sheikh wa Mkoa wa Dodoma, Mustapha Rajabu, akizungumza na Nipashe, alisema anampongeza Ndugai kwa uamuzi wake wa kuachia nafasi ya ubunge kwa hiari jambo ambalo limekuwa gumu kwa wanasiasa wengi nchini.

Alisema uamuzi huo unapaswa kuigwa na wabunge wengine kwa kuwa amefanya jambo sahihi ambalo litampatia sifa kwa wananchi wake ambao walimchagua kuwaongoza kwa zaidi ya miaka 20.

"Maoni yangu kwa Ndugai ni kumpongeza tu kwa uamuzi wake. Kitendo alichofanya ni cha kizalendo, kiungwana na kinampatia heshima badala ya kusubiri hadi kuondolewa kwa aibu," alisema.

Pia alisema jambo ambalo amelifanya Ndugai litamfanya aendelee kukumbukwa na watu wengi kwa kuwa amefanya uamuzi kama huo pia alipotangaza kuachia nafasi ya uspika kwa hiyari yake.




Ofisa Rasilimali Watu wa Kampuni ya Barrick, Alfa Rashid (kushoto), akibadilishana mawazo na watendaji kutoka Taasisi ya AIESEC, Heritha Godfrey (kulia) na Hytham Jacob, katika kongamano la kuwajengea uwezo wanafunzi lililofanyika katika Chuo Kikuu cha Mzumbe mkoani Morogoro juzi kwa udhamini wa kampuni hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shekhe ataka maimamu, walimu wa madrasa kutatua migogoro

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SHEKHE wa Mkoa wa Dodoma, Mustafa Rajabu, amewaagiza maimamu na walimu wa madrasa wa kata na mitaa Jiji la Dodoma, kuhakikisha wanatatua na kuondoa migogoro inayoweza kuhatarisha amani kwa waumini.

Rajab alitoa agizo hilo kupitia ziara yake ya kukagua majengo ya misikiti na madrasa yaliyoko kwenye kata na mitaa.

Akizungumza kwenye ziara hiyo na maimamu na walimu wa madrassa, alisema viongozi hao wanatakiwa kuondoa migogoro ambayo inajitokeza kwenye misikiti yao.

Ili wafanikiwe katika hilo, alisema ni muhimu kwenye ibada zao wakadumisha na kufundisha amani, umoja, mshikamano na upendo.

Pia aliwataka wasimamizi wa majengo ambayo yamechakaa kuhakikisha wanashirikiana na waumini wao kuyajenga mapya badala ya kuendelea na magofu hayo.

Alisema bado kuna baadhi ya majengo ya misikiti na madrasa yaliyo mengi kwenye kata na mitaa ya jiji la Dodoma yanahitaji kujengwa upya kutokana na kuchakaa.

Shekhe Rajabu alitumia nafasi hiyo kuwakumbusha waumini wa dini hiyo kuendelea kudumisha ibada ambazo walizokuwa wakizifanya katika kipindi cha mwezi wa Ramadhani.

Sambamba na hilo, aliwataka viongozi na waumini kushiriki kutoa majibu sahihi ya takwimu pale sensa ya watu na makazi itakapofanyika Agosti, mwaka huu.

Alisema hiyo ni pamoja na familia ambazo zinaishi na watu wenye ulemavu na vikongwe kutowaficha kwa kuwa na wao wanahitajika kuhesabiwa kama ilivyo kwa wengine wasio na ulemavu.





# Miundombinu ya Nanenane Mbeya yakabiliwa uchakavu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAANDALIZI ya Maonyesho ya Wakulima maarufu Nanenane kwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini yameanza kufanyika jijini Mbeya huku kukiwa na tatizo la uchakavu wa baadhi ya miundombinu uliosababishwa na maonyesho hayo kutofanyika mwaka jana.

Maonyesho ya Nanenane ambayo hufanyika kikanda kila mwaka nchi nzima, kwa mwaka jana hayakufanyika kutokana na uwepo wa mlipuko wa ugonjwa wa UVICO -19 hali iliyosababisha serikali kuyasitisha ili kuzuia msongamano wa watu usiokuwa wa lazima.

Hata hivyo, serikali imeruhusu maonyesho hayo yaendelee kufanyika kuanzia mwaka huu, ambapo viongozi, wataalamu na wakulima kutoka mikoa saba ya Nyanda za Juu Kusini walikutana jana jijini Mbeya kuanza maandalizi.

Kikao cha maandalizi ya maonyesho hayo kilifanyika katika viwanja vya John Mwakangale ambavyo hutumika kwa ajili ya maonyesho ya Nanenane kwa Nyanda za Juu Kusini, chini ya Uenyekiti wa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera.

Akifungua kikao hicho, Homera alisema maonyesho ya mwaka huu ni lazima yawashirikishe wakulima wengi kuanzia ngazi ya kata hadi kikanda ili wajifunze mbinu na teknolojia bora za kilimo.

"Tunahitaji maonyesho ya wakulima ya mwaka huu yawe ya kipekee. Tunapaswa kuwashirikisha wakulima wenyewe kuanzia ngazi za chini kabisa ili wajifunze mbinu za kilimo bora, teknolojia na aina ya pembejeo zinazofaa ili kuongeza tija kwenye kilimo," alisema Homera.

Alisema kuwa umuhimu wa kila halmashauri kutoka mikoa yote ya Nyanda za Juu Kusini kuwaandaa wakulima kuanzia ngazi ya kata, wilaya na hatimaye kanda ili wafike kwenye maonyesho hayo na kuonyesha au kujifunza mbinu bora za kilimo na ufugaji.

Homera aliongeza kuwa katika maonyesho hayo pia ziwapo ngoma za asili za watu wa Nyanda za Juu Kusini kwa ajili ya burudani na pia kuhamasisha utalii kwa mikoa hiyo.

Akizungumzia hali ya uwanja wa maonyesho hayo, Mwakilishi wa Katibu Tawala Mkoa wa Mbeya, Donard Bombo, alisema baadhi ya miundombinu ya uwanja huo imechakaa na kutokana na kutofanyika kwa maonyesho hayo mwaka jana kwa sababu ya uwepo wa changamoto ya UVIKO- 19.

"Kutokana na maonyesho ya wakulima kutofanyika mwaka jana kwa sababu ya uwapo wa changamoto ya ugonjwa wa korona (UVICO -19), kwa sasa maeneo ya uwanja ni machafu, maana kuna vichaka na nyasi ni ndefu. Lakini mabanda mengi yamechakaa, rangi zimepauka na hata hali ya miundombinu kama vile barabara si ya kuridhisha," alisema Bombo.

Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga, alisema uamuzi wa serikali kurejesha maonyesho hayo ni fursa nzuri kwa wakulima na wananchi wengine kukuza uchumi wao, hivyo ni muhimu maandalizi yake yakawa mazuri ili kuleta tija iliyokusudiwa.

Alisema maonyesho hayo yataamsha tena ari na chachu ya wakulima katika kuendeleza kilimo na kuzalisha kwa tija.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Waziri Kindamba, alisema umakini unahitajika katika matumizi ya fedha wakati wa maandalizi ya maonyesho hayo ili kusiwapo na ubadhirifu wa aina yoyote na hatimaye maonyesho yafanyike kwa tija.



Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, akizungumza na wanachama wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT), Wilaya ya Chunya, mkoani Mbeya juzi, kabla ya kuwakabidhi msaada wa mashine ya kusagia mawe ya dhahabu 'Karasha' kwa ajili ya kutumika kama kitega uchumi cha umoja huo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wachimbaji watakiwa kujiandaa kwa sensa

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

SERIKALI wilayani Chunya, imewataka wachimbaji wadogo wa madini kujiandaa kushiriki kwenye sensa ya watu na makazi inayotarajiwa kufanyika Agosti 23, mwaka huu, nchini kote.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Simon Mayeka, aliyasema hayo juzi alipokuwa akizindua utoaji elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kushiriki kwenye sensa hiyo na kumtaka kila mmoja kushiriki.

Alisema asilimia kubwa ya wachimbaji wadogo wilayani hapa wana tabia ya kuhamahama kutoka sehemu moja kwenda nyingine na kwamba endapo wataendelea na utaratibu huo, kuna uwezekano wasishiriki tukio hilo muhimu kwa maendeleo ya nchi.

Katika kipindi hiki cha kuelekea kwenye sensa, alisema wananchi wote wanatakiwa kusitisha uhamaji ili wakutwe na maofisa wa sensa kwenye maeneo yao na wahesabiwe.

Mayeka alisema sensa ya watu na makazi ni muhimu kwa ajili ya kuisaidia serikali kupanga mipango ya kuwahudumia wananchi, hivyo akawataka kila mmoja kujiandaa kuhesabiwa.

"Hata wafugaji wetu mnatakiwa msihamehame katika kipindi hiki maana mnaweza mkaathiri hili jambo. Kila mmoja akutwe kwenye eneo lake ili ahesabiwe. Hii itatusaidia pia kupata takwimu sahihi hata za wafugaji," alisema Mayeka.

Pia aliwataka wananchi kupuuzia upotoshaji unaoenezwa na baadhi ya watu kuhusu sensa wakihusisha na baadhi ya vitu ambavyo si sahihi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Tamim Kambona, alisema kwa sasa wanaendelea na maandalizi ya sensa ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa viongozi wa ngazi mbalimbali kabla ya kuingia kwa wananchi.

Alisema wanawashirikisha viongozi wote wa serikali ngazi za chini, viongozi wa dini na viongozi wa mila ili na wao washiriki kwenye uhamasishaji wa wananchi wanaoishi nao kwenye maeneo yao.

# Wanafamilia wanusurika kifo kwa moto

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATU wanne wa familia moja, wamenusurika kifo baada ya nyumba yao kuteketea kwa moto katika Mtaa wa Ishinga Kata ya Iganjo jijini Mbeya huku mali zote zilizokuwa ndani zikiteketea, hivyo kuiacha familia hiyo bila makazi.

Walionusurika na ajali hiyo ni Suzzy Mwakasege na watoto wake watatu ambao kwa mujibu wa maelezo ya mama huyo, nyumba hiyo ilishika moto wakati yeye na wanawe wakiwa wako kwenye biashara.

Akizungumza juzi wakati wa kupokea misaada mbalimbali kutoka kwa wadau, Suzzy alisema alikuwa kwenye biashara na watoto lakini baada ya kuona muda umekwenda aliamua kuwapakia watoto kwenye gari ili watangulie nyumbani.

Alisema wakati anaendelea na biashara alipigiwa simu na majirani wakimweleza kwamba nyumba inawaka moto na ndipo akaamua kufunga biashara na kuwahi.

Mwakasege alisema bahati nzuri ni kwamba watoto nao walikuwa bado kufika nyumbani, hivyo aliwakuta njiani wakiwa wanakwenda nyumbani na alipofika nyumbani, alikuta moto mkubwa ukiwa unazimwa na majirani.

"Nawashukuru majirani zangu walijitahidi kuzima moto japokuwa vitu vyangu vote vilivyokuwamo viliteketea. Nililazimika kukodi pikipiki kutoka kibandani kuja hapa nyumbani na watoto niliwakuta njiani wameshuka kenye daladala wanatembea kwenda nyumbani," alisema.

Mwakasege aliwaomba wasamaria wema waendelee kumshika mkono ili kuirejesha nyumba yake katika hali ya kawaida kwa maelezo kuwa nyumba haikuanguka licha ya bati zote kuteketea.

Wadau mbalimbali walijitokeza kuifariji familia hiyo kwa kutoa msaada wa vitu mbalimbali ikiwamo chakula, nguo na vifaa mbalimbali vya ujenzi kwa ajili ya kurejesha miundombinu ya nyumba hiyo katika hali yake ya kawaida.

Mbunge wa Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson, ambaye ni Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitoa mabati 32 yenye thamani ya Sh. 800,000 kwa familia hiyo kwa ajili ya kuezeka nyumba ya familia hiyo.

Akikabidhi msaada huo, Katibu wa Mbunge, Joseph Chambanenge, aliwapa pole wanafamilia wa familia hiyo pamoja na wakazi wa Mtaa wa Ishinga kutokana na tatizo hilo la ajali ya moto.

Alisema ofisi ya mbunge ilipata taarifa ya kutokea kwa ajali hiyo na ndio maana ikaamua kutoa msaada huo hasa ikilenga kuezeka nyumba ili kuipunguzia gharama familia hiyo.

"Mbunge wenu anawapa pole sana wanafamilia kwa tatizo lililotokea na ametutuma tuje tuwapatie mabati haya ili yawasaidie kupunguza gharama za ujenzi, lakini tunawaomba wadau wengine waendelee kuisaidia familia hii," alisema Chambanenge.

Meneja wa Taasisi ya Tulia Trust, Jacqueline Boaz, aliwashauri wanawake kuwa makini wakati wa kupika kwa maelezo kuwa chanzo cha moto ulioteketeza nyumba hiyo ulisababishwa na jiko la mkaa walilokuwa wameinjikia maharage.



# Nishati salama kuokoa mazingira Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KUPATIKANA kwa nishati salama Zanzibar kutaokoa matumizi makubwa ya kuni na kuhifadhi mazingira ikiwamo misitu kwa kuwa asilimia 90 ya wananchi wa vijijini wanatumia kuni kwa ajili ya kupikia.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar, Sheha Mjaja Juma, wakati akizungumza na waandishi wa habari kando ya mkutano wa sekta ya nishati uliofanyika katika Hoteli ya Madina tul Bahari mjini Zanzibar.

Mkutano huo ambao uliwashirikisha wadau wa maendeleo pamoja na watendaji wa serikali wa sekta ya nishati ulikuwa na lengo la kuiwezesha Zanzibar kuwa na njia mbadala ya matumizi ya nishati.

Mkurugenzi huyo alisema kuni zinazotumiwa na wananchi kwa ajili ya kupikia zinatoka katika misitu na kwa mwaka wastani wa hekta 500 za msitu zinakatwa, hivyo kuwa na nishati salama ikiwamo ya jua itawezesha wananchi kuitumia na kutaokoa matumizi makubwa ya kuni na hatimaye kuhifadhi misitu.

"Nishati inayotokana na kuni moshi wake ni hatari kwa afya za wananchi. Wanawake ndio waathirika zaidi kutokana kuwa wao ndio watumiaji wakubwa wa kuni kwa ajili ya kupikia. Kuwapo kwa nishati mbadala kutaimarisha afya zao," alisema.

Pia alisema nishati salama ikiwamo ya jua husaidia kuhifadhi mazingira hasa misitu ambayo husaidia kufyonza hewa ukaa ambayo inasababisha mabadiliko ya tabianchi.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini, Dk. Mgereza Miraji Mzee, alisema serikali iko katika mchakato wa kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umeme kwa sababu Zanzibar inategemea umeme kutoka Tanzania Bara. Katika kufanya hivyo, alisema mkakati ni kuwa na chanzo cha uzalishaji wa umeme kinachozalishwa Zanzibar kikiwamo umeme jua.

"Mikakati ya serikali ya Zanzibar ni kuwa na umeme wa jua wa migawati 18 ambao ni kama asilimia 25 ya umeme unaotumika utazalishwa Zanzibar," alisema.

Katibu Mkuu huyo alisema mabadiliko ya tabianchi na hali ya hewa yanaathiri kwa kiwango kikubwa nishati ya umeme kwa sababu Zanzibar inatumia waya ambao hupita chini ya bahari kwa ajili ya usafirishaji umeme kutoka Tanzania Bara.

"Bahari ina changamoto nyingi katika mambo ya mabadiliko ya hali ya hewa, hivyo hatutaki tusubirie litokee la kutokea kisha tuanze kuhangaika. Ili kutatua tatizo hilo, tumeona tuwe na njia ya uzalishaji wa umeme wa jua na upepo," alisema.

Naye Waziri wa Maji, Nishati na Madini, Shaibu Hassan Kaduwara, alisema wadau wa maendeleo wameisaidia Zanzibar katika maeneo mbalimbali ikiwamo mradi wa nishati ya jua ya kilowati 80 kwa kisiwa cha Kokota Pemba na sasa wananchi wa kisiwa hicho wanatumia nishati hiyo na kilowati 50 kwa Kisiwa cha Njau, Pemba.

Aliwataja baadhi ya wadau hao wa maendeleo ni serikali ya Norway ambayo imesaidia upatikanaji wa umeme wa jua katika visiwa hivyo pamoja na Benki ya Dunia katika utekelezaji wa mradi wa megawati 18 za umeme wa jua unaojengwa kijiji cha Makunduchi, Kusini Unguja.

Pia alisema washirika hao wa maendeleo watasaidia katika kutatua changamoto ya uchakavu wa miundombinu ya umeme ambapo watasaidia kubadilisha nguzo chakavu za umeme 400 kwa Unguja na 1000 kwa Pemba na unafuu wa kuunganisha umeme pamoja na bei nafuu ya umeme kwa wananchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania, (JET), John Chikomo, aliipongeza serikali ya Zanzibar katika juhudi zake za kupambana na uhifadhi wa mazingira ikiwamo uzalishaji wa nishati ya umeme wa jua ambayo ni nishati rafiki kwa mazingira.

"JET tunaunga mkono juhudi za serikali katika kupambana na uhifadhi wa mazingira hasa katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Baadhi ya maeneo ya Unguja na Pemba yameanza kuvamiwa na maji ya bahari na serikali imefanya juhudi za kujenga ukuta ili kupunguza athari za mabadiliko hayo," alisema.

## Waziri akiri kuwapo udhalilishaji wanandoa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, amesema kumekuwa na udhalilishaji mkubwa wa wanandoa sambamba na talaka holela Zanzibar.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali aliloulizwa na Mwakilishi wa Konde, Zawadi Amour, aliyetaka kujua kwa kuwa kumekuwa na udhalilishaji mkubwa wa wanandoa na talaka za papo kwa papo, kwa nini mafunzo ya ndoa yasiwe lazima kwa kila mwanandoa.

Kutokana na kuwepo kwa hali hiyo, alisema lazima kupata mafunzo ya ndoa kwa kila mwanandoa kabla ya kuoa na kuolewa ili kuzinusuru ndoa na kupunguza wajane na watoto wanaoishi na mzazi mmoja.

"Hili ni jambo jema lakini inatubidi tufanye maandalizi ya kisheria kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji bora wa jambo hilo," alisema.

Alisema hadi kufikia Aprili, mwaka huu, wanaume 810 sawa na asilimia 37 na wanawake 1,358 sawa na asilimia 63 wamepatiwa mafunzo hayo ya ndoa.

Mafunzo hayo ya ndoa, alisema yanatolewa kwa wanaume na wanawake walioko katika ndoa na ambao hawako katika ndoa kwa kuzingatia maombi ya kujiunga na mafunzo hayo, yaliyopokewa katika mafunzo hayo kwa kutumia walimu wanaume na wanawake.

Pia alisema utaratibu wa mafunzo ya ndoa unaanzia kwa kuchukua fomu za maombi ya kujiunga na mafunzo zinazotolewa bure kwa mwananchi yeyote anayetaka kupatiwa mafunzo hayo kama ilivyo, katika aina zingine za mafunzo yanayotolewa na taasisi zingine.



Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Simai Mohamed Said, akizungumza wakati wa kipindi cha maswali na majibu katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani nje ya Mji wa Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# AG ataka kasi kesi za udhalilishaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MWANASHERIA Mkuu wa Serikali Zanzibar, Dk. Mwinyi Talib Haji, amesema vyombo vinavyosimamia sheria ikiwamo Mahakama Kuu na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) vihakikishe kesi za udhalilishaji wa kijinsia zinasikilizwa kwa kasi na kutolewa hukumu zinazostahiki kwa mujibu wa sheria.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akitoa ufafanuzi wa majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kusimamia taasisi zilizo chini yake zinazosimamia mwenendo wa haki, sheria na mashauri ya jinai.

Dk. Mwinyi alisema katika kipindi cha mwaka mmoja, zaidi ya mashauri ya kesi za udhalilishaji wa kijinsia 160 zimesikilizwa katika mahakama mbalimbali za Unguja na Pemba na kutolewa hukumu.

Alisema kesi 30 watuhumiwa wake wametiwa hatiani na kutumikia vifungo zaidi ya miaka 13 jela ikiwa ni sehemu ya mikakati ya kushughulikia kesi za udhalilishaji wa kijinsia.

Mwanasheria mkuu alitaja baadhi ya marekebisho makubwa yaliyofanywa katika vyombo vya sheria ni pamoja na kuifanyia marekebisho Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ambayo imepinga kutoa dhamana kwa watuhumiwa makosa ya udhalilishaji wa kijinsia ikiwamo ubakaji.

"Nataka niwaambie wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba tumefanya maboresho makubwa katika vyombo vya sheria vinavyoshughulikia mwenendo wa makosa ya jinai zaidi katika matukio ya kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia," alisema.

Pia alisema kwa mujibu wa maelekezo yaliyotolewa na serikali, watendaji wa vyombo vya sheria wametakiwa kuharakisha mwenendo wa kesi na kuweka muda wa miezi mitatu kuhakikisha upelelezi wa kesi unakamilika.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## TANGAZO

**KERO YA MTARO ULIOCHIMBWA MBELE YA NYUMBA YANGU KIWANJA NO. 94 BLOCK 8 KATA YA KAMBI TANO MTAA CAPE TOWN,S.L.P147 MOROGORO**

**WEMA KARIM MMBAGA**

Mtajwa hapo juu ni mkazi wa lukobe mkoani morogoro kata ya kambi tano mtaa wa cape town ni mjane.Naomba serikali kunipatia ufumbuzi wa haraka juu ya mtalo wa maji machafu uliochimbwa mbele ya nyumba yangu na kusababisha kero ya muda mrefu kwa wakazi wa eneo hilo,natumai selikari yangu nisikivu na itanipatia ufumbuzi juu ya Kero hii.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**
**MAOMBI MADOGO NAMBA 59 YA 2022**
**ISDORI TAVE..........MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**UFUNUO ISRAEL, MSIMBE RAJABU, IDRISA ABDUL MBONDE,**
**ANITA J.MFELEJI, MOHAMED IBLAIM, MATESO SIAGA ......WAJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA**

**MSIMBE RAJABU** popote ulipo Mnaarifiwa ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro tarehe 31/05/2022 mbele ya Mwenyekiti **E.MOGOSA** wewe mwenyewe binafsi au utume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa.Endapo hautahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi

Imetolewa kwa **MKONO** wangu na MUHURI Baraza leo tarehe 10/05/2022.

**E. MOGASA**
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)**
**MOROGORO**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**(MCA/84)**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya MIKUMI**
**Wilaya ya KILOSA**

**MADAI NAMBA ...... 41..... YA......2022**
**MDAI: MIKUMI CREDIT LTD**
**MDAIWA: CHRISANTUS ADRIAN MTANGA**
**MADAI: FEDHA TSH 2,366,665/=**
**KWA: CHRISANTUS ADRIAN MTANGA**

Unaamrishwa na JAMHURI uhudhurie mbele ya mahakama hii siku ya JUMATANO tarehe 08/06/2022 saa2.30 asubuhi kuwa ni mdaiwa katika shauri lililotajwa hapo juu na ukifika usiondoke bila ya ruhusa ya mahakama , na unaonywa kwamba ukiwa utapuuza wito huu bila ya udhuru wa maana hati itatolewa kukulazimisha kuhudhuria

Hati hii inatolewa kwa amri yangu na muhuri wa Mahakam ahii leo 05/05/2022

Kuitwa shaurini hii imetolewa kwa maombi ya **MIKUMI CREDIT LTD**

MIKUMI CREDIT LTD

MAHAKAMA YA MWANZO MIKUMI KILOSA - MOROGORO

Hakimu wa Mahakama ya mwanzo

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO 53 OF 2022**

**In the Matter of the Estate of the Late PAULO MAURICE MASENEKA**

**By 1. ANJERIKA PAULO MASENEKA**
**2. EVARIST SIMON SANDAWE**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above –named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 31st day of MAY ..... 2022

Dated at MOROGORO this 10 day of MAY ...2022

RESIDENT MAGISTRATE

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT COURT
P.O. Box 660, Morogoro

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**LEILA MRISHO LUPINDA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1247-0029** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia shule ya sekondari **ST. MARKS SECONDARY SCHOOL** mwaka 2018. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/URA/RB/174926/2022**

---

## TANGAZO LA MNADA

Work ethic company limited Kwa idhini tuliyopewa na FANIKIWA MICROFINANCE COMPANY tunapenda kuutarifu umma kuwa Tutafanya mnada wa hadhara wa Nyumba na viwanja katika maeneo tofauti katika jiji la Dar es salaam ,Wateja wanashauriwa kulipa madeni yao ndani yasiku 14 kutoka tarehe ya hili Tangazo vinginevyo Mnada utaendelea kama Tarehe za Mnada Zinavyoonekana hapa chini.

| Jina la mdaiwa | Mahali dhamana ilipo | Tarehe ya mnada |
|---|---|---|
| Conjestar L awrence Kaugala | Kiwanja chenye je ngo kipo chanika | 25.05.2022 |
| Imelda Adam Lyanzile | Nyumba ipo kifuru | 26.05.2022 |
| Frola Honest Mosha | Nyumba ipo luguluni Ubungo | 27.05.2022 |
| Prosper Faustin Tarimo | Nyumbo ipo Ngoma mapindunzi kigamboni | 28.05.2022 |
| Regnat January Kassian | Nyumba ipo kichangani kigamboni | 28.05.2022 |
| Benjamini Matiko Chacha | Nyumba ipo kigamboni Mkwajuni | 28.05.2022 |
| Ally Nassoro Kimbugu | Nyumba ipo Temeke kwa Nyoka | 29.05.2022 |

**Masharti ya Mnada.**

1. Mnunuzi atakeyeshinda atalipa 25%(au Zaidi) ya bei iliyofikwa kwenye mnada na salio la (75%)litalipwa ndani ya siku kumi nne(14) kuanzia tarehe ya mnada.
2. Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa mda uliotolewa atakuwa amepoteza haki zote na mali itauzwa upya.
3. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe yaTangazo.

**Kwa mawasiliano piga 0717956315 (Workethic) au 0623662447 (Workethic) au 0677014355(Fanikiwa)**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MWANGA**

**UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**SHAURI LA MIRATHI NA 3 YA MWAKA 2022**

**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIAJI WA MIRATHI YA GERVAS ABDALLAH MSANGI..................MAREHEMU**

**FULGENCE GERVAS MSANGI....................MUOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewakwa barua za usimamiaji wa mirathi kwa muombaji aliyeomba hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikwa mnamo au kabla ya tarehe **16 Mwezi Mei, Mwaka 2022** Imewasilishwa Mwanga leo tarehe **09 Mwezi wa Mei Mwaka 2022**

DISTRICT COURT MWANGA

HAKIMU MKAZI MWANDAMIZI
MAHAKAMA YA WILAYA MWANGA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Njombe**

**Kituo cha Njombe Mjini**
**Mkoa Njombe**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 36/2022**

**Katika Shauri la Mirathi ya**

**HELFRIDA SEVELINI MSIGWA....................Marehemu**
**Wa N.H.C – Njombe.**

**Katika Shauri la Maombi ya kumteua Msimamizi yaliyotolewa na ANNA RASHIDI NGIGWA**

**TANGAZO LA UMMA**

**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 09 Mwezi wa 06 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa kabla au mpaka tarehe tajwa hapo juu. **Zingatia;** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo tarehe 9 Mwezi wa 5 Mwaka 2022.

HAKIMU MKAZI

---


***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

# Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0782253676**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Putin ajiandaa kwa vita vya muda mrefu

**WASHINGTON,** MAREKANI

RAIS wa Russia, Vladmir Putin anajiandaa kwa vita vya muda mrefu nchini Ukraine, hata ushindi unaopatikana katika eneo la mashariki hautamaliza mzozo huo.

Idara ya kijasusi ya Marekani imetoa onyo hilo, wakati mapigano makali yakiendelea katika eneo la mashariki, ambako Russia inajaribu kulichukua.

Russia ilielekeza nguvu mpya kwa wanajeshi wake kuteka eneo la Donbas baada ya Ukraine kukataa majaribio ya kuchukua mji mkuu wake wa Kyiv.

Taarifa kutoka idara hiyo ya ujasusi ilisema vikosi vyake vimesalia katika mkwamo.

Avril Haines, mkurugenzi wa ujasusi wa kitaifa, aliiambia kamati ya Seneti ya Marekani juzi kuwa Putin bado ana nia ya kufikia malengo zaidi ya Donbas, lakini kwamba anakabiliwa na kutofautiana kati ya matarajio yake na uwezo wa sasa wa kijeshi wa kawaida wa nchi yake.

Aliongeza kuwa kiongozi huyo alikuwa akitegemea msaada wa Marekani na EU kwa Ukraine kudhoofika huku mfumuko wa bei, uhaba wa chakula na bei ya nishati ikizidi kuwa mbaya.

Hata hivyo, anaweza kugeukia njia kali zaidi huku vita vikiendelea ingawa ingetumia tu silaha za nyuklia ikiwa Putin ataona tishio lililopo kwa Russia.

Mkurugenzi wa Shirika la Ujasusi la Ulinzi Scott Berrier aliambia kikao hicho kwamba Warrusia na Waukraine walikuwa katika mkwamo kidogo.

Katika mapigano ya hivi karibuni , Ukraine inadai kutwaa tena makazi manne katika eneo la kaskazini-mashariki la Kharkiv.

Cherkasy Tyshky, Ruski Tyshky, Rubizhne na Bayrak yote yalinyakuliwa kutoka kwa Russia, vikosi vya silaha vya Ukraine vilisema.

Rais Volodymyr Zelensky, alisema mafanikio ya nchi yake yanasukuma hatua kwa hatua vikosi vya Russia kutoka Kharkiv, ambayo imekuwa ikishambuliwa tangu vita hivyo vianze.

Marekani yadai Russia imerusha makombora ya kasi 10

WIZARA ya Ulinzi ya Pentagon, ilisema inaamini Russia imetumia silaha zake za kasi ya hypersonic takriban 10 hadi 12 tangu kuanza kwa vita nchini Ukraine.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, ofisa huyo alisema Marekani haina hesabu kamili ya makombora yaliyotumika.

Russia inadai kuwa kombora la Kinzhal ambalo linaweza kulenga shabaha hadi kilomita 2,000 sawa na maili 1,240 linaweza kuruka kwa kasi ya zaidi ya kilomita 6,000 kwa saa, lilirushwa kwa mara ya kwanza kwenye shabaha nchini Ukraine mwezi Machi.

Hivi karibuni, maofisa wa Ukraine walidai kuwa silaha hiyo ilitumiwa huko Odesa mwishoni mwa juma.

Ofisa huyo wa Marekani, hata hivyo, alisema kuwa hana chochote cha kuashiria kwamba zilitumiwa dhidi ya sehemu zilizokuwa zinalengwa katika jiji hilo.

Hungary yapinga vikwazo vya mafuta

Umoja wa ulaya unalenga kupiga marufuku kabisa uagizaji wa mafuta kama sehemu ya vikwazo zaidi dhidi ya Russia. Lakini sio kila mwanachama wa umoja wa Ulaya (EU) anaunga mkono hatua hiyo.

Nchi mwanachama Hungary ilisema vikwazo vya mafuta dhidi ya Russia vitaharibu uchumi wa nchi hiyo.

Waziri wa Mambo ya Nje Peter Szijjarto, alisema Tume ya Ulaya haina suluhu la matatizo makubwa ambayo yatajitokeza kwa nchi yake, licha ya mazungumzo ambayo yamekuwa yakifanyika.

Akinukuliwa na Reuters, kiongozi huyo alisema kuwa makubaliano kuhusu vikwazo vya mafuta vitafanya kazi tu ikiwa vitaelekezwa kwenye usafirishaji wa mafuta ya baharini, na usafirishaji wote kupitia mabomba hali itakuwa mbaya.

## Mshambuliaji wa kijihadi ahusika na shambulio

**MOGADISHU,** SOMALIA

BOMU la kujitoa mhanga limelipuliwa katika mji wa Mogadishu nchini Somalia, likilenga kituo cha ukaguzi kwenye barabara inayoelekea uwanja wa ndege

Kundi la wanamgambo wa Kiislamu, al-Shabab, limedai kutekeleza shambulio hilo.

Siku ya Jumapili, wabunge wanatazamiwa kumchagua rais mpya wa nchi hiyo.

Kura hiyo, ambayo imeahirishwa mara kadhaa, itafanyika ndani ya jumba la ndege kwenye uwanja wa ndege. Hata hivyo, wapiganaji wa Al-Shabab hufanya mashambulizi mara kwa mara katika mji huo.

Mlipuaji huyo wa kujitoa mhanga alikufa katika tukio hilo na ilielezwa alikuwa akilenga magari yaliyokuwa katika kituo cha ukaguzi cha barabara kuu ya kuelekea uwanja wa kimataifa wa ndege wa Aden Adde.

Shambulio hilo linasemekana kusababisha majeruhi kadhaa, wakiwemo wanajeshi na raia, kwa mujibu wa vyanzo vya ndani.

Eneo hilo liko chini ya kilomita tano kutoka uwanja wa ndege, ambapo wagombea wanaowania kiti cha urais wanatarajiwa kutoa hotuba zao za kampeni Bungeni.

Ujumbe wa kulinda amani wa Umoja wa Afrika umeweka marufuku ya kutotoka katika eneo la kambi ya jeshi la anga la Afisyoni huko Hangara na maeneo ya jirani.

Kuna wagombea 39 wanaowania uchaguzi wa urais wa Somalia, ambapo uchaguzi huo umecheleweshwa kwa zaidi ya mwaka mmoja, kutokana na ukosefu wa usalama nchini humo.

Mwezi uliopita, shambulio la risasi lilikatiza kikao cha bunge ambapo walilengwa wabunge wapya walioapishwa waliokuwa wameketi.




Waandishi wa habari wakiomboleza kifo cha mwanahabari mwenzao Shereen Abu Aqleh wa kituo cha Al Jazeera, ambaye ameuawa kwa kupigwa risasi alipokuwa akiripoti kuhusu uvamizi wa vikosi vya usalama vya Israel katika mji wa Jenin, Ukingo wa Magharibi. **PICHA BBC**

## Wahamiaji Uingereza wajificha kukwepa kupelekwa Rwanda

**LONDON,** UINGEREZA

WAHAMIAJI ambao wanaomba hifadhi nchini Uingereza, wameamua kujificha kwa kuhofia kupelekwa nchini Rwanda kwa ajili ya makazi mapya.

Mashirika ya misaada yalisema kwamba waomba hifadhi kadhaa wamejificha kwa sababu ya hofu kuwa watasafirishwa hadi Rwanda kutokana na mashariti mapya.

Chini ya mkataba uliotiwa saini mwezi uliopita, watu wanaohukumiwa kuingia nchini kinyume cha sheria wanakabiliwa na kupelekwa Rwanda kwa ajili ya kupata makazi mapya.

Shirika la Msalaba Mwekundu na Baraza la Wakimbizi lilisema tishio la kuondolewa limewafanya baadhi ya wale wanaotafuta hifadhi kujidhuru na mmoja amejaribu kujiua.

Mashirika ya kutoa misaada yamekosoa mipango ya serikali ya Uingereza kuwa ni ukiukaji wa wajibu wa kutoa huduma.

**Habari zote BBC**

# MBEYA CITY YAPANIA NAFASI YA KUCHEZA MICHUANO CAF

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuifumua Azam FC mabao 2-1 kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya juzi, Kocha Mkuu wa Mbeya City, Mathias Lule, amesema mipango yake sasa ni kushinda michezo mitatu ijayo, miwili ikiwa ya nyumbani akitafuta pointi sita na tatu za ugenini.

Michezo miwili watakaocheza nyumbani katika Uwanja wa Sokoine ni dhidi ya Polisi Tanzania na Yanga, huku wakiwa na kibarua kigumu ugenini dhidi ya KMC FC, Ruvu Shooting na Simba.

Akizungumza na gazeti hili jana, Lule alisema mechi zimekuwa na ushindani mkubwa na wanapambana kutafuta matokeo katika michezo mitano ya ijayo kwanza kwa kuhakikisha wanapata pointi sita katika mechi mbili za nyumbani.

Alisema pointi sita hizo anahitaji kuzipata dhidi ya Polisi Tanzania Jumapili wiki hii na kisha watakapoikaribisha Yanga Juni 19, mwaka huu.

"Kutafuta pointi tatu nyumbani ni muhimu sana, jana (juzi), tumechukuwa kwa Azam FC, wanakuja Polisi Tanzania halafu tunaenda kucheza ugenini huko tunapambana kutafuta pointi tatu ila tukipata moja si mbaya.

"Tukimalizana na Polisi tunaenda kucheza na KMC FC, Ruvu Shooting halafu tunaenda kucheza na Simba baada ya hapo tutawakaribisha Yanga nyumbani," alisema Lule.

Alisema ana matarajio makubwa ya kufanya vizuri katika michezo hiyo mitano ili kufikia malengo yao ya msimu huu, kumaliza katika nafasi ya nne ambayo watakuwa miongoni mwa timu zitakazokwenda kushiriki michuano ya kimataifa.

Lule alisema malengo yao ni kushiriki michuano ya kimataifa, hivyo wanalazimika kupambana kutafuta matokeo katika michezo iliyopo mbele yao ili kujiweka katika nafasi nzuri katika msimamo wa ligi hiyo.

Matokeo chanya dhidi ya Azam FC juzi, yanaifanya Mbeya City sasa kufikisha pointi 31 katika nafasi ya nne baada ya kushuka dimbani mara 23.



Mratibu wa onyesho la 'Wafia Dansi', Benard James, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuhusu maandalizi ya onyesho hilo. Kulia ni Rais wa Bendi ya Mjengoni Classic ya Arusha, Digital Mukongya, Rais wa Bendi ya Waluguru Original ya Morogoro. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# BASATA yawafunda wanavyuo

**Na Saada Akida**

BARAZA la Sanaa la Taifa (BASATA), limewataka wanafunzi vyuoni kutumia vema thamani ya vipaji vyao vizuri na kuviendeleza kwa kuwa sanaa ni kazi nzuri itakayowasaidia katika kufikia malengo yao katika maisha.

Ushauri huo ulitolewa jana na Ofisa Mwandamizi wa BASATA, Agustino Makame, wakati wa utoaji zawadi kwa washindi watatu wa shindano la 'Unitalante' ambalo lilifikia tamati wiki iliyopita.

Washindi hao wa kwanza ni kikundi cha kucheza dansi, African Cousins kutoka Kituo cha Taasisi ya Sanaa Bagamoyo (TASUBA), ambacho kilizawadiwa Sh. milioni 10, nafasi ya mshindi wa pili ikienda kwa Afro Dreams, kilichoibuka na Sh. milioni tano na Osman Soka ambaye alikuwa mchekeshaji akizawadiwa na Sh. milioni moja kwa kuibuka mshindi wa tatu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Makame alisema malengo ya shindano hilo yalikuwa ni kuibua vipaji mbalimbali vya sanaa kwa wanafunzi wa vyuo.

Alisema zawadi wanazopewa ni ili kuongeza thamani yao, lakini vipaji vyao ndiyo kitu kikubwa zaidi, hivyo wanapaswa kuviendeleza kwa sababu sanaa ni kazi lakini ni biashara.

"Kuwapo kwa mashindano ya kusaka vipaji ikiwamo ya 'Unitalent' ni ishara tosha kuwa wanafunzi vyuoni wana uwanja mpana wa kuonyesha vipaji vyao na kuviendeleza na hatimaye kupeperusha vema bendera ya burudani," alisema Makame.

Naye Mkurugezi wa Kampuni iliyoandaa shindano hilo, Chrispine Kiondosha, alisema wanafanikiwa kukamilisha msimu wa tatu wa shindano hilo na kuwakabidhi zawadi zao.

Alisema shindano hilo litakuwa endelevu kwa lengo la kuendeleza vipaji kwa wanafunzi vyuoni na kuhakikisha wanakwenda kuviendeleza ili kufikia malengo yanayotarajiwa.

"Sanaa ni biashara, lakini kazi kama ilivyo zingine kwa sababu tunaona sanaa kwa sasa inavyofanya vizuri katika anga za kimataifa," alisema Kiondosha.

# Warriors Queens yaendeleza ubabe

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Warriors Queens, imeendelea kujiimarisha kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ya Wanawake Zanzibar baada ya juzi kuimiminia mvua ya mabao 16-0 timu ya Dunga Queens katika mwendelezo wa ligi hiyo kwenye hatua hii ya lala salama.

Kwa matokeo hayo, Warriors Queens imeendelea kung'ang'ania usukani katika msimamo wa ligi hiyo yenye timu 10 kwa kufikisha alama 30 baada ya michezo 11 iliyocheza hadi sasa.

Warriors mpaka sasa ndio timu ambayo haijapoteza mchezo tangu kuanza kwa msimu wa ligi hiyo ya Wanawake ambayo inachezwa katika viwanja vya Unguja na Pemba.

**Kwa upande wa wapinzani wao, timu ya New Generation nao katika mchezo wa 11 walifanikiwa kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Yellow Queens, hivyo kuendelea kushika nafasi ya pili kwa alama 27 huku wakiwa wamepoteza mechi moja hadi sasa.**

# Makalla aalikwa usiku 'Wafia Dansi'

**Na Sabato Kasika**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika onyesho maalum liitwalo 'Wafia Dansi', litakalofanyika mwishoni mwa mwezi huu jijini Dar es Salaam likishirikisha bendi tano.

Hayo yalisemwa na mratibu wa onyesho hilo, Benard James, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana na kufafanua kuwa linalenga kufufua muziki wa dansi ambao kwa sasa umeyumba.

"Tumemualika mkuu wa mkoa wa Dar es Salaam na viongozi wengine wa wizara inayohusika na sanaa na kama hawatapata nafasi, basi mkuu wa mkoa wa Dar es Salaam atakuwa mgeni rasmi," alisema James.

Mratibu huyo alitaja bendi zitakazotoa burudani kwenye onyesho hilo kuwa ni Msondo Ngoma, Bogos Musica, Mapacha Music zote za Dar es Salaam, Waluguru Original ya Morogoro na Mjengoni Classic ya Arusha.

"Sasa ni mwaka wa pili tukiendelea na juhudi za kuburudisha muziki huu wenye hadhi yake kama ilivyokuwa miaka ya nyuma, tunaomba vyombo vya habari vitusaidie katika juhudi hizi," alisema.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### COUTINHO AWANIWA NEWCASTLE
KLABU ya Newcastle United imezungumza na Philippe Coutinho kujaribu kuipiku Aston Villa katika mbio za kumsajili kiungo huyo Mbrazil kwa mkataba wa kudumu kutoka Barcelona. ***(Goal)***

### WATKINS ATAJWA WEST HAM
WEST Ham inamwania mshambuliaji wa Aston Villa na England, Ollie Watkins mwenye umri wa miaka 26, huku klabu hiyo ya Midlands ikitarajiwa kutaka pauni milioni 50 ili kumwachia. ***(Guardian)***

### AZPILICUETA HAKIELEWEKI BARCA
BARCELONA ipo tayari kumpa mshahara mnono wa pauni milioni 11 kwa mwaka nahodha wa Chelsea, Cesar Azpilicueta, lakini wanatatizwa na kanuni za fedha, hivyo hawataweza kumpa mshahara mnono mlinzi huyo wa Hispania. ***(Goal)***

### RUDIGER SAFI MADRID
REAL Madrid imeweka pauni milioni 340 kwenye mkataba wa Antonio Rudiger akitaka kuuzwa huku mlinzi huyo wa Ujerumani akisaini mkataba wa miaka minne ambao unamfanya alipwe pauni 315,000 kwa wiki akitokea Chelsea bure. ***(Mail)***

### TIELEMANS KUONDOKA LEICESTER
KLABU ya Leicester City inatarajia kiungo wake, Youri Tielemans ataondoka mwishoni mwa msimu na wanajiandaa kusikiliza ofa ya angalau pauni milioni 40 kwa ajili ya nyota huyo mwenye miaka 25 ambaye mkataba wake unamalizika mwaka 2023. ***(90 Min)***

### ARSENAL KWA TIELEMANS
ARSENAL ni moja ya klabu zinazohusishwa na Youri Tielemans, lakini matumaini yao ya kumnasa yatategemea kama watamaliza nne bora kwenye Ligi Kuu England na kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao. ***(Standard)***

### OSIMHEN AWINDWA UNITED
MANCHESTER United na Newcastle United wanamtaka mshambuliaji, Victor Osimhen, lakini Napoli inataka angalau pauni milioni 85.5 ili kumwachia nyota huyo mwenye umri wa miaka miaka 23. ***(Calciomercato, via Football Italia)***

### LOTITO NA MILINKOVIC-SAVIC
RAIS wa Lazio, Claudio Lotito amesema alikataa ofa ya pauni milioni 120 kwa ajili ya kiungo wa Serbia Sergej Milinkovic-Savic, 27 anayewaniwa na Manchester United na Paris St-Germain. ***(Rai Sport, via Talksport)***

### INACIO AWANIWA UNITED
MANCHESTER United iko tayari kulipa pauni milioni 38 kwa ajili ya mlinzi wa Sporting Lisbon, Goncalo Inacio mwenye umri wa miaka 20. ***(A Bola)***

### PEPE ATAJWA SEVILLA
KLABU ya Sevilla wanaweza kumsajili winga wa Arsenal, Nicolas Pepe mwenye umri wa miaka 26, mwishoni mwa msimu, huku thamani ya nyota huyo wa kimataifa wa Ivory Coast ikitajwa kushuka hadi pauni milioni 25. ***(Super Desporte, via Mirror)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MANE AZIGONGANISHA BAYERN MUNICH, BARCA

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Senegal ameripotiwa kuwa anataka kuhama pale Anfield huku akiwa...

**LIVERPOOL, England**

KLABU ya Barcelona imejitosa kuwania saini ya Sdio Mane wa Liverpool huku pia taarifa zikieleza kuwa Bayern Munich nao wanamtaka mchezaji huyo, kwa mujibu wa Mundo Deportivo.

Mane amekuwa akitajwa kuwa mmoja wa wachezaji ambao wana nafasi ya kuwania taji la Ballon d'Or katika wiki za hivi karibuni.

Na mshambuliaji huyo wa Liverpool pia uvumi umekuwa ukizagaa kuhusu mustakabali wake ndani ya timu hiyo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, aliisaidia Senegal kushinda Kombe la Mataifa ya Afrika Februari mwaka huu na amefunga mabao 15 kwenye Ligi Kuu England.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Senegal ameripotiwa kuwa anataka kuhama pale kwenye viunga vya Anfield huku akiwa amebakiwa na miezi 12 ya mwisho kwenye mkataba wake.

Barcelona wamemkosa mchezaji wa Borussia Dortmund, Erling Haaland ambaye atajiunga na Manchester City na wamedhamiria kupata mshambuliaji mahiri katika msimu huu wa majira ya joto.

Wakati Barca wakimfikiria Mane, miamba ya Bavaria, Bayern nayo imeripotiwa kuingia kwenye mbio za kuwania saini ya nyota huyo wa Liverpool.


LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,255

MECHI KALI
TOTTENHAM
VERSUS
ARSENAL
1 | 2.10
X | 3.42
2 | 3.22

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# KLOPP ATIA NENO USAJILI WA HAALAND MAN CITY



**LIVERPOOL, England**

JURGEN Klopp anaamini kuwa Manchester City "haiwezi kushinda kitu" kwa sababu ya ubora binafsi wa Erling Haaland, kwani itamboresha zaidi mchezaji huyo na si vinginevyo.

Wapinzani hao wa Liverpool katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu England, walithibitisha Jumanne kwamba, wamefikia makubaliano kimsingi na Borussia Dortmund kwa ajili ya kumsajili Haaland.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, amefunga mabao 28 katika mechi 29 alizoichezea Dortmund mwaka huu na anatarajiwa kutua City, ambao walikuwa wakihusishwa vikali na Harry Kane mwaka jana.

Na Klopp ameibuka na kusema kwamba, Haaland ni kipaji kisichopingika na asili ya uchezaji wa City chini ya Pep Guardiola inamaanisha wana uwezekano mkubwa wa kumbadilisha mshambuliaji huyo wa Norway kuliko kumzoea.

"City haikuwahi na haitakuwa timu ambayo itashinda mechi kwa sababu ya mchezaji mmoja," alisema Klopp aliwaambia waandishi wa habari baada ya timu yake ya Liverpool kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Aston Villa, Jumanne kwenye mchezo wa Ligi Kuu.

"Kuna njia maalum ya kucheza, na nadhani Erling atatambua kuwa atafunga mabao mengi. Lakini atabadilishwa zaidi.

"Atapenda hilo, lakini Man City watamboresha zaidi yeye kuliko kumtegemea kwa kuwawezesha kushinda mataji."

Liverpool wamelingana kwa pointi na City kwa muda kileleni mwa msimamo baada ya ushindi huo wa Jumanne pale Villa Park, lakini mabingwa hao watetezi jana, Jumatano walikuwa wanacheza na Wolves.

# Aubameyang: Naamini Dembele atabaki Barca

**BARCELONA, Hispania**

PIERRE-Emerick Aubameyang anatumai "kwa moyo wangu wote" Ousmane Dembele atasaini mkataba mpya wa kubakia Barcelona.

Dembele yuko ndani ya wiki chache za mwisho za mkataba wake na amekuwa akipendekezwa sana kujiunga na klabu nyingine kama mchezaji huru.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa, aliambiwa hadharani kuondoka Barca na klabu hiyo wakati wa dirisha la uhamisho la Januari baada ya mazungumzo kuhusu mkataba mpya kuvunjika.

Lakini baada ya kuwa nje kwa majeruhi, Dembele amerudi ndani ya kikosi akiwa mmoja wa wachezaji muhimu zaidi kwa 'Blaugrana' hao kwa kipindi cha miezi minne iliyopita.

Hakika, baada ya kutengeneza mabao mawili katika ushindi wa 3-1 Jumanne dhidi ya Celta Vigo, Dembele sasa amesaidia kufunga mabao 13 kwenye LaLiga msimu huu.

Hiyo ni pamoja na pasi za mabao 11 pekee tangu mwanzoni mwa mwaka, ambazo ni mbili zaidi ya mchezaji mwenzake wa zamani Lionel Messi kama ndiye aliyeongoza Ligi Kuu tano za Ulaya mwaka 2022.

Aubameyang alipata asisti nyingine kati ya hizo dhidi ya Celta na amemtaka Dembele, ambaye aliungana naye Borussia Dortmund, abaki Camp Nou.

"Ni mdogo wangu," alisema Aubameyang akiiambia Movistar+.

"Tumekuwa pamoja kwa muda mrefu, tangu siku ya kwanza alipowasili Dortmund.

"Baada ya muda tumejenga uhusiano huu wa ndugu, ndiyo maana nampenda sana.

"Anaendelea vizuri sana sasa na nina furaha sana kwa ajili yake. Natumaini kwa moyo wangu wote kwamba atabaki."

Dembele ni mmoja wa wachezaji watatu wa Ufaransa tangu msimu wa 2006-07 kutoa pasi za mabao 13 au zaidi katika msimu mmoja katika ligi tano bora za Ulaya, pamoja na Kylian Mbappe na Christopher Nkunku.

Aubameyang aliifungia Barca mabao mawili baada ya Memphis Depay kufunga bao la kwanza, kabla ya bao la Ia Aspas kuonekana kuwapa njia Celta ya kurejea kwenye mechi.

Hilo lilikuwa bao la 10 kwa Aspas katika mechi 15 za LaLiga dhidi ya Barcelona, idadi ambayo ni Diego Forlan pekee ndiye anaweza kufikia dhidi ya wababe hao wa Katalunya kwenye ligi hiyo karne hii.

5,316,060

JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 14/05/22 | 20:00 | Niort vs Valenciennes | 2.42 | 3.18 | 2.83 |
| 02. 14/05/22 | 20:00 | Nancy vs PAU FC | 2.34 | 3.27 | 2.88 |
| 03. 14/05/22 | 20:00 | Nimes vs Bastia | 2.57 | 3.16 | 2.67 |
| 04. 14/05/22 | 22:00 | Bordeaux vs Lorient | 2.29 | 3.49 | 2.84 |
| 05. 14/05/22 | 22:00 | Toronto FC vs Orlando City | 2.45 | 3.44 | 2.78 |
| 06. 14/05/22 | 22:30 | Colorado Rapids vs Los Angeles FC | 2.39 | 3.57 | 2.77 |
| 07. 15/05/22 | 13:30 | Bologna vs Sassuolo | 2.58 | 3.47 | 2.48 |
| 08. 15/05/22 | 16:00 | Leeds vs Brighton | 2.34 | 3.33 | 2.83 |
| 09. 15/05/22 | 16:00 | Watford vs Leicester | 2.77 | 3.52 | 2.30 |
| 10. 15/05/22 | 16:30 | St. Pauli vs Fortuna Dusseldorf | 2.28 | 3.56 | 2.77 |
| 11. 15/05/22 | 16:30 | Sandhausen vs Holstein Kiel | 2.62 | 3.47 | 2.44 |
| 12. 15/05/22 | 18:30 | Degerfors vs Helsingborg | 2.44 | 3.22 | 2.63 |
| 13. 15/05/22 | 19:30 | Villarreal vs Real Sociedad | 2.31 | 3.56 | 2.80 |

MECHI ZA USHINDI
"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 12/05/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 5868 | KMC vs Mtibwa Sugar | 2.04 | 2.73 | 4.10 |
| 15:00 | 3957 | Ofspor vs Fethiyespor | 2.33 | 3.16 | 2.82 |
| 15:00 | 5571 | Orduspor 1967 vs Icel Idmanyurdu Spor | 2.60 | 3.04 | 2.60 |
| 16:00 | 1082 | Ofta de Kribi vs New Star | 2.66 | 2.76 | 2.76 |
| 16:00 | 1238 | Sivas Dort Eylul vs Bodrumspor | 2.02 | 3.31 | 3.31 |
| 16:00 | 1831 | Artvin Hopaspor vs Kutahyaspor | 2.88 | 2.92 | 2.44 |
| 16:00 | 2096 | Ethiopia Bunna SC vs Wolkite City FC | 2.18 | 2.81 | 3.49 |
| 16:00 | 4358 | Bayburt Idare vs Duzyurtspor | 2.26 | 3.25 | 2.86 |
| 16:00 | 5491 | Ruvu Shooting vs Geita Gold FC | 2.32 | 2.73 | 3.31 |
| 16:00 | 5672 | Yafoot Yaounde vs Union de Loum | 3.61 | 3.07 | 2.01 |
| 17:00 | 2351 | Sogdiyona Jizzax vs Nasaf Qarshi | 2.41 | 2.82 | 3.02 |
| 17:00 | 4969 | Pakhtakor vs Surkhon Termez | 1.10 | 7.22 | 18.53 |
| 17:30 | 1315 | Fovu De Baham vs Avion Academy | 3.54 | 2.91 | 2.11 |
| 17:30 | 4691 | Dragon FC Yaounde vs Cotonsport | 3.84 | 3.40 | 1.84 |
| 18:00 | 2790 | KuPS Kuopio vs Haka | 1.55 | 3.70 | 5.45 |
| 18:00 | 3173 | PWD Bamenda vs Bamboutos | 2.28 | 2.82 | 3.26 |
| 18:00 | 3224 | Renaissance de N. vs Eding Sport FC | 4.86 | 2.96 | 1.80 |
| 18:00 | 5087 | Lahti vs HJK Helsinki | 5.67 | 3.91 | 1.50 |
| 18:00 | 5932 | Karabakh vs FK Sumgayit | 1.08 | 7.96 | 21.37 |
| 19:00 | 1475 | Odense vs Viborg FF | 2.16 | 3.40 | 3.15 |
| 19:00 | 5952 | Vejle BK vs Aarhus | 2.39 | 3.43 | 2.74 |
| 19:20 | 1129 | Al Taawon vs AL Baten | 1.77 | 3.75 | 4.20 |
| 19:30 | 2230 | Universitatea Craiova vs Sepsi Osk | 1.77 | 3.07 | 4.77 |
| 19:30 | 2263 | Lyngby vs Hvidovre IF | 1.62 | 3.79 | 4.56 |
| 20:00 | 1397 | Norresundby BK vs Vejgaard B | 3.85 | 4.40 | 1.72 |
| 20:00 | 1506 | Real Sociedad vs Cadiz CF | 1.67 | 3.60 | 5.19 |
| 20:00 | 2312 | Tromso vs Valerenga | 2.29 | 3.43 | 2.88 |
| 20:00 | 2568 | VSK Arhus vs IF Lyseng | 1.60 | 4.20 | 4.80 |
| 20:00 | 2698 | Isparta 32 Spor vs Bursa Niluferspor | 2.50 | 2.94 | 2.79 |
| 20:00 | 3035 | Fuglebakken Kfum vs ASA Aarhus | 2.48 | 3.79 | 2.31 |
| 20:00 | 3137 | Viking vs Stromsgodset | 1.49 | 4.58 | 5.37 |
| 20:00 | 4591 | Tarsus vs Amedspor | 1.79 | 3.31 | 4.18 |
| 20:00 | 5313 | Frederikssund vs Alleroed FK | 2.60 | 3.80 | 2.38 |
| 21:00 | 3615 | Midtjylland vs Brondby | 1.55 | 4.08 | 5.38 |
| 21:00 | 4493 | Rayo Vallecano vs Villarreal | 4.19 | 3.59 | 1.81 |
| 21:30 | 1219 | Vicenza vs Cosenza | 2.02 | 3.17 | 3.71 |
| 21:30 | 1267 | FC Zurich vs Lausanne-Sport | 1.33 | 5.36 | 7.34 |
| 21:30 | 1738 | Renate vs Juventus U23 | 2.15 | 3.15 | 3.15 |
| 21:30 | 2881 | Queens Park vs Airdrieonians | 2.33 | 3.34 | 2.80 |
| 21:30 | 2954 | Palermo vs Triestina | 1.82 | 3.35 | 3.98 |
| 21:30 | 4424 | Anderlecht vs Royal Antwerp | 1.55 | 4.19 | 5.18 |
| 21:30 | 5564 | FC Basel vs Grasshoppers | 1.76 | 3.73 | 4.18 |
| 21:30 | 5601 | Feralpisalo vs Pescara Calcio | 2.01 | 3.20 | 3.45 |
| 21:30 | 5648 | Virtus Entella vs Foggia | 2.10 | 3.20 | 3.20 |
| 21:45 | 1268 | Dartford vs Chippenham Town | 1.50 | 4.10 | 5.27 |
| 21:45 | 1688 | Tottenham vs Arsenal | 2.10 | 3.42 | 3.22 |
| 21:45 | 2879 | Kidderminster vs Boston Utd | 2.03 | 3.30 | 3.30 |
| 21:45 | 3521 | Cesena vs Monopoli | 1.84 | 3.32 | 3.90 |
| 22:15 | 1947 | Keflavik IF vs Leiknir | 1.98 | 3.60 | 3.16 |
| 22:30 | 5721 | Real Madrid vs Levante | 1.51 | 4.61 | 5.27 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# SIMBA QUEENS YABAKIZA POINTI 3 KUPEWA KOMBE

**Na Adam Fungamwango**

NI pointi tatu tu inatakiwa kuzipata timu ya soka ya Wanawake ya Simba, Simba Queens kuweza kutawazwa tena kuwa mabingwa wa Ligi Kuu Wanawake nchini kwa msimu wa tatu mfululizo, baada ya juzi kuichapa The Tigers Queens mabao 3-0 kwenye Uwanja wa Braeburn International School jijini Arusha.

Yalikuwa ni mabao ya wachezaji wa kimataifa, Warundi Asha Djaffar na Joelle Bukuru, pamoja na Mkongomani Pambani Kuzoya, yaliyotosha kuwaweka karibu na ubingwa msimu huu.

Timu hiyo ambayo imecheza mechi 19 na kubakisha michezo mitatu, inahitaji pointi hizo ili zifikie 57 ambazo hazitaweza kufikiwa na timu yoyote ile wakati huu ikiwa imeshafunga mabao 88 na kufungwa sita.

Timu za Fountain Gate Princess na Yanga ambazo zote zimeshinda mechi zao za juzi, zitafikisha pointi 56 kama zitashinda mechi tatu zilizobaki kila moja, kwani zina pointi 47.

Yanga Princess iliitwanga Oysterbay Girls mabao 3-0 kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, mawili yakitumbukizwa nyavuni na Aisha Juma, huku moja likifungwa na Mkongomani Olga Tshilombo, wakati Fountain ikiichakaza Alliance Girls mabao 2-0 kwenye Uwanja wa Nyamagana, Mwanza.

Matokeo ya mechi zingine zilizochezwa juzi ni Ilala Queens iliokiona cha moto kwa kufungwa nyumbani, Uwanja wa Karume, mabao 3-0 dhidi ya Ruvuma Queens, huku 'dabi' ya mkoani Pwani kati ya Mlandizi Queens na JKT Queens, ikimalizika kwa sare ya mabao 2-2.




Kikosi cha Simba Queens, ambacho kimebakiza pointi tatu katika mechi tatu kabla ya kutawazwa kuwa mabingwa wa msimu wa 2021/22 wa Ligi Kuu Bara. **PICHA: SIMBA**

# Mayanga aipania KMC Uhuru leo

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI leo ikiwa na shughuli pevu ugenini katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam dhidi ya KMC FC, Klabu ya Mtibwa Sugar imesema itawakosa nyota wake watatu kutokana na sababu mbalimbali.

Akizungumza na gazeti hili jana akiwa njiani kuelekea Dar es Salaam baada ya gari yao kuharibika, Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Salum Mayanga, alitaja wachezaji watakaoukosa mchezo huo kuwa ni Abdi Banda ambaye ana matatizo ya kifamilia, Jofrey Luseke pamoja na Ibrahim Ame ambaye aliungana na wenzake kambini jana.

"Tumejipanga vizuri kukutana na timu ya KMC japo wapo nyumbani, hatuwezi kukubali kupoteza mchezo wetu huo," alisema Mayanga.

Alisema licha ya kuwakosa wachezaji hao hakuna kitakachoharibika kwani wana kikosi kipana ambacho anaimani nacho.

Alisema wachezaji wote morali ya yao ipo juu kuelekea mchezo huo, wakiwa na lengo la kushinda na kushika nafasi ya juu katika msimamo wa Ligi Kuu mwishoni mwa msimu.

Mayanga alisema anashukuru kuona raundi hii ya lala salama timu yake imeanza kubadilika, baada ya kupata matokeo mazuri katika michezo yao waliyoicheza hivi karibuni.

Kabla ya mchezo wa jana kati ya Polisi Tanzania na Dodoma Jiji uliopigwa Uwanja wa Ushirika mjini Moshi, Mtibwa Sugar ilikuwa nafasi ya tisa ikiwa na pointi 27 zilizotokana na mechi 22, wakati KMC ambayo nayo imeshuka dimbani kwa idadi hiyo ya michezo, ikiwa katika nafasi ya 11 na alama zake 24.

Michezo
Alhamisi Mei 12, 2022
Nipashe





## Mane azigonganisha Bayern, Barca

# NABI AGEUKIA SAFU YAKE YA USHAMBULIAJI

●●●Ni kuelekea mechi ya Dodoma Jiji, asema jukumu la kufunga si la Mayele pekee, ataka...

**Na Saada Akida**

WAKATI mzimu wa sare ukikiandama kikosi chake kwa sasa, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema ana jukumu kubwa la kuhakikisha anapambana kufanyia kazi udhaifu uliojitokeza katika safu yake ya ushambuliaji ili kuweza kufanikisha ushindi katika michezo iliyopo mbele yao hususan ni ujao wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Dodoma Jiji FC.

Hatua hiyo ya Nabi imekuja baada ya Yanga kuandamwa na sare tasa tatu mfululizo, huku washambuliaji wake wakishindwa kutumia nafasi wanazozitengeneza.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema ameona mapungufu ya kikosi chake na anayafanyia kazi ikiwamo safu ya ushambuliaji kuwa makini na kuhakikisha wanatumia vema nafasi wanazotengeneza.

Sare za Yanga zilianza katika mechi yake ya nyumbani Uwanja wa Benjamin Mkapa dhidi ya Simba na kisha kwenda kulazimishwa suluhu tena ugenini kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mjini Kigoma dhidi ya Ruvu Shooting kabla ya kurejea dimba la Mkapa na kutoka suluhu dhidi ya Tanzania Prisons.

Nabi alisema katika safu ya ushambuliaji haitakiwi kumtegemea Fiston Mayele pekee, kwani kila mmoja ndani ya timu hiyo ana jukumu la kufunga ili kuhakikisha wanapambania matokeo.

"Hizi mechi tulizokosa ushindi tulicheza vizuri na nafasi tulitengeneza ila tulikosa umakini, hivyo tunafanyia kazi ili kuhakikisha tunaenda kupambana kutafuta ushindi katika michezo iliyopo mbele yetu," alisema Nabi.

Alisema kazi kubwa aliyoifanya ni kurejesha morali kwa wachezaji wake kuhakikisha wanapambana kutafuta matokeo chanya katika michezo iliyopo mbele yao ukiwamo dhidi ya Dodoma jiji FC Jumapili wiki hii katika Uwanja wa Jamhuri, Dodoma.

Nabi alisema ana matumaini makubwa na kikosi chake kufanikiwa kutimiza malengo yao ya kutwaa ubingwa huo kwa kuhakikisha wanapata matokeo mazuri katika michezo iliyopo mbele yao.

"Kama nilivyosema awali kwamba hakuna mechi iliyo rahisi kwetu hasa katika hizi timu zilizopo chini ya msimamo zinapokutana na Yanga, michezo iliyobaki tunaenda kucheza kama fainali ili kufikia malengo yetu ya kutwaa ubingwa wa ligi," alisema Nabi.

Pamoja na sare hizo, Yanga bado haijapoteza mchezo wowote na ipo kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 57 baada ya mechi 23, ikifuatiwa na Simba yenye alama 46 kabla ya mchezo wake wa jana dhidi ya Kagera Sugar.



Morrison

## Simba yafunguka kuondoka Morrison

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imewataka wanachama na mashabiki wao kupuuza taarifa na tetesi za mitandaoni kuwa mchezaji wao, Bernard Morrison ataondoka mwishoni mwa msimu huu.

Kwa wiki nzima sasa kumekuwa na tetesi kwenye mitandao mbalimbali ya kijamii hasa ya michezo, ikidai kuwa mchezaji huyo aliyesajiliwa na timu hiyo kutoka Yanga miaka miwili iliyopita, huenda akarejea huko.

Pia tetesi hizo hizo zinadai kuwa huenda klabu ya Simba ikaamua kuachana naye.

Lakini Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally, ameweka wazi kuwa hakuna yeyote anayejua mpaka sasa nani atabaki na nani ataondoka kwenye klabu hiyo, mpaka hapo Kocha Mkuu, Pablo Franco atakapotoa ripoti yake baada ya msimu kumalizika, itakayoainisha nani anataka aendelee kuwa naye na yupi hamhitaji.

"Hizo tetesi za Morrison au Onyango kuhusu kuondoka zinabaki kuwa tetesi, kwetu sisi nani anaondoka, nani atabaki, ukifika muda sahihi kila kitu kitawekwa wazi na atakayebaki na kuondoka itakuwa ni kwa matakwa ya Kocha Mkuu, Pablo Franco.

**"Wapo wachezaji ambao wamaliza mikataba yao ndani ya Simba, kubaki au kuondoka kunategemea na ripoti ya mwalimu, akisema nani anamtaka tutambakisha, akisema mchezaji fulani simhitaji, hata kama ana mkataba tutauvunja na kumpa mkono wa kwa kheri, Simba tumeshawahi kufanya hivyo.**

"Atakayeondoka ataondoka kwa matakwa ya mwalimu kwa sababu ya kuona kuwa hatomsaidia na atakayebaki, atabaki kwa sababu ataona anafaa, hakuna anayejua nani atasalia nani atabaki, tunamwachia kocha, na hizo zote ni tetesi," alisema Ahmed.

Morrison na Onyango ni kati ya wachezaji wanaomaliza mikataba yao ndani ya klabu hiyo na bado inaelezwa hakujafanyika mazungumzo mapya.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >